UKURASA 20



**Maskini Angella augua ugonjwa usiojulikana**

## Wabunge walilia barabara kuepusha vifo vya wajawazito



UKURASA 5

# MAISHA

FEBRUARI 21, 2021 Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Ukurasa 10
**Kweli dada wa kazi amemuweza mwanao?**



Ukurasa 15
**MAISHA NI NYUMBA**
Kuwa makini unapotafuta nyumba ya kuishi



**HARUSI**
Ukurasa 12



bo


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Februari 21, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580498


# Majaliwa: Serikali haijazuia barakoa



**Aagiza** zivaliwe kujikinga na maradhi, ataka watu kufuata masharti ya afya ... *Endelea uk. 2*



Mawaziri wakiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, baada ya mazishi kwenye makaburi ya Kanisa Katoliki la Mtakatifu Augustino, eneo la Manundu, wilayani Korogwe, mkoani Tanga jana. Kutoka (kushoto) ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maji Juma Aweso, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Ummy Mwalimu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekinolojia Prof. Joyce Ndalichako na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Jenista Mhagama. **PICHA: OWM**

## Laini za simu kuwa na neno la siri

UKURASA 3



# Hofu ya njaa yaibuka nzige kuvamia mazao

UKURASA 3

**MICHEZO** **KOCHA AL AHLY ATAO UTABIRI MECHI SIMBA** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Majaliwa asema serikali haijazuia kuvaa barakoa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali haijakataza uvaaji wa barakoa na kusisitiza zivaliwe katika shughuli za kutoa huduma kwa watu walio ndani ya umbali wa chini ya mita moja.

Majaliwa aliyasema hayo jana katika misa ya kuaga mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, iliyofanyika Korogwe mkoani Tanga kabla ya maziko yaliyofanyika siku hiyo.

"Nimeona leo (jana) tabia ambayo tuliizungumza hata mwaka jana. Watu wana tabia ya kunawa, wananawa kwa kutumia kitakasa mikono (sanitizers), wengine wamevaa barakoa.

"Barakoa utaivaa pale ambako unajua shughuli zako siku hiyo zitakupelekea (zitakusababishia) kupata au kutoa huduma na wengine walioko ndani ya umbali wa chini ya mita moja ambako kunapunguza hatari ya kutema mate, unyevunyevu. Hapo unaweza kuvaa hakuna aliyekataza, muhimu kila mmoja aende kwa tahadhari," alisema.

Majaliwa aliwasihi Watanzania wakati dunia ikiwa kwenye mahangaiko ya maambukizi ya maradhi mbalimbali, wawe watulivu na kwamba serikali inawapenda.

"Tumejikita kuhakikisha tunafuatiliana kuona mwenendo wa magonjwa haya. Tuna magonjwa mengi, tuna malaria, UKIMWI, tuna shinikizo la damu, sukari, magonjwa chungu nzima. Wataalam wetu kwenye hospitali, maabara wanaendelea na uchunguzi na kujikita kutoa huduma. Rais ametusihi kipindi hiki, tuendelee kuzingatia masharti ya afya," alisema.

Juzi, Rais John Magufuli aliwaomba Watanzania kuondoa hofu na kuwataka viongozi wa dini kuongoza kufunga siku tatu na kuendelea na maombi.

"Ninawashukuru nimeshuhudia jana (juzi) swala za Ijumaa wameanza kutekeleza kwa kuzungumza na waumini kuliombea taifa. Hata leo (jana) Wasabato nimeona kwenye vyombo vya habari walioko kanisani wanaliombea taifa. Ninaomba Baba Askofu nanyi muwe na maandalizi ya kuliombea taifa kesho (leo)," alisema.

Majaliwa alisema wamesikia kwenye mitandao kila mmoja anasema lake na wale wenye simu zinazoonyesha taarifa wameona mataifa mbalimbali yakieleza hiyo ni vita iliyoanza kwa wakubwa na bado wanahangaika nayo.

"Mataifa madogo lazima tuwe makini. Bahati nzuri tuna Rais makini sana na ameendelea kutuongoza vizuri ametusihi tuondoe hofu, muhimu ndani tunaendelea kupambana kuhakikisha usalama wa watu wetu unaendelea kuwapo.

"Barakoa mnazozivaa wakati huo tulisema ni bora tukajiridhisha zinatoka wapi. Bora ukatengeneza yako au iliyotengenezwa Tanzania. Barakoa ni nguo inayozuia mate yasitoke au ukapokea vitu vingine. Tumeona hata kwenye mitandao wakieleza hili na lile, lazima tuwe makini na tufuate masharti ya afya," alisisitiza.

KIJAZI AENZIWE

Majaliwa alisema wanalo jukumu kubwa la kumuenzi Kijazi hasa watumishi wa umma wameachiwa somo zuri kwa yale mema aliyoyatenda wakati wa utumishi wake.

"Kwa yote mema yaliyotamkwa na viongozi mbalimbali wakiwamo wa serikali, Bunge na viongozi wa dini, jukumu la kumuenzi ni letu sote hatuna namna ametuachia misingi imara," alisema.

Majaliwa aliwashukuru viongozi wa dini kwa kazi kubwa wanayoifanya na kuwaeleza kuwa serikali inatambua mchango wao wanaoutoa kulifanya taifa kuwa tulivu na watu wake waendelee kushirikiana.

Naibu Spika wa Bunge, Tulia Ackson, akizungumza kwa niaba ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitoa pole kwa familia na ndugu na kueleza kuwa Balozi Kijazi si tu ametoa mchango kwa serikali na Bunge bali pia kwa kanisa.

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, alisema wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama walikuwa karibu na Balozi Kijazi ambaye pia alikuwa Katibu wa Baraza la Usalama na wao ni wajumbe.

"Kabla ya kwenda kujadiliwa kwenye Baraza la Usalama, ilikuwa lazima zichambuliwe na sekretarieti ambayo yeye alikuwa mwenyekiti wetu. Tulikuwa karibu sana katika kuratibu masuala yote ya usalama wa nchi na alikuwa mahiri akiongoza kwa upole, unyenyekevu, weledi mkubwa na tulinufaika kwa kuishi kwake duniani," alisema Jenerali Mabeyo kwa niaba ya wakuu wa vyombo vya usalama.

Alisema ameibua utashi wa namna gani na wao wataishi kwa weledi na kutaka waliobaki watafakari wanaishi au wanakuwepo duniani.




MWONEKANO WA KITUO KIKUU CHA MABASI YA MIKOANI NA NCHI JIRANI CHA MBEZI MWISHO, JIJINI DAR ES SALAAM, BAADA YA KUWEKWA MAANDISHI YA KUKITAMBULISHA. **PICHA: MIRAJI MSALA**



## Dk. Likwelile afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa zamani wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Servecius Likwelile, amefariki dunia.

Taarifa iliyotolewa jana na mke wake, Vicky Kamata, ilithibitisha kifo cha kiongozi na mwanataaluma huyo kwamba alikutwa na mauti akiwa nyumbani kwao, Mbweni, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Hata hivyo, Kamata hakueleza kama Dk. Likwelile (pichani) alikuwa anaumwa au la.

Dk. Likwelile alikuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kuanzia mwaka 2013 hadi Agosti 21, 2016 Rais John Magufuli alipotangaza kutengua uteuzi wake na kwamba angepangiwa kazi nyingine. Nafasi yake ilichukuliwa na James Dotto.

Likwelile ambaye kabla ya kutumika katika nafasi mbalimbali serikalini, alikuwa Mhadhiri Mwandamizi Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hadi mwaka 2001 alipoteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Kuondoa Umaskini katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Baada ya hapo, aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Ofisi ya Rais.

Kutokana na utendaji kazi wake mzuri, Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, alimteua kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha (wakati huo) mwaka 2011 kabla ya kumpandisha na kuwa Katibu Mkuu.

# Diwani aangua kilio kutaka Zahanati kijijini

**Na Stevie Chindiye, Tunduru**

DIWANI wa Viti Maalum Tarafa ya Matemanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Sharifa Nico, juzi aliangua kilio wakati akiomba halmashauri kukamilisha ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Mtangashari, kata ya Ligunga, ili kuwarahisishia upatikanaji wa huduma za afya.

Akizungumza kwa uchungu, diwani huyo alisema ni kipindi chake cha tatu kuingia katika Baraza la Madiwani na amewasilisha kilio cha wananchi hao kwa muda mrefu bila mafanikio.

Nico alisema wananchi walijitolea kufyatua matofali zaidi ya mara tatu na yaliyatumia kujenga majengo ambayo yalibomoka na matofali mengine zingine kuota vichuguu.

Kutokana na hali hiyo, diwani huyo aliwaomba watendaji wa halmashauri hiyo kutembelea eneo hilo ili kuangalia uwezekano wa kukamilisha ujenzi wake ili nguvu za wananchi zisipotee bure.

"Kila mwaka wa uchaguzi tumekuwa tukiahidi kwa wananchi wa kijiji hicho kuwa zahanati hiyo tutaikamilisha na mara kadhaa imewahi kupangiwa fedha na baadaye kubadilishiwa matumizi," alisema huku akitokwa na machozi.

Aidha, madiwani wengine waliwalalamikia wataalamu wa halmashauri hiyo kwa kubadilisha na kutopeleka fedha za miradi ambayo hupitishwa katika kipindi cha zaidi ya miaka mitano.

Mmoja wa madiwani hao, Nakoko Bazil, wa kata ya Mindu, alidai kuondolewa Sh. milioni 95 zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo, nyumba ya mwalimu na jengo la utawala katika shule ya sekondari ya kata hiyo.

Naye Diwani wa Mbesa, Daniel Mlanda, alilalamikia utaratibu wa wataalamu kubadilisha majina ya shule 11 zilizopangiwa kupelekewa miradi ya ujenzi wa matundu ya vyoo kwa zaidi ya Sh. milioni 200.

Diwani wa Tinginya, Aliasa Mshamu, alidai Sh. milioni 30 zilizopangwa kujengewa ghala la kuhifadhia mazao ziliondolewa huku Diwani wa Ngapa, Said Pindu, akilalamikia kutopatiwa mradi yoyote mbali na eneo lake kuchimbwa madini kwa miaka mingi.

Naye Diwani wa Viti Maalumu wa Tarafa Nampungu, Rehema Nyoni, alilalamika halmashauri kuondoa Sh. milioni 15 zilizo kuwa zimepangwa kuboresha bwawa la kijiji cha Kidodoma.

Akijibu kwa nyakati tofauti kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Ofisa Mipango alisema kuwa miradi mingi imekwama kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa halmashauri hiyo.

Awali, akichangia hajo hiyo, Mbunge wa Tunduru Kusini, Daimu Mpakate, aliwataka madiwani kushirikiana na watendaji wao katika maeneo yao kuainisha vyanzo vipya vya mapato na kuhakikisha kuwa fedha zinakusanywa.

Akitoa salamu za serikali, Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, alimtaka Mkurugenzi Mtendaji kufanya mapitio na uhakiki wa leseni za wafanyabiashara na kuona kama zinazotumika ndizo walizoombea kufanyia biashara husika.

Mtatiro alisema ili kudhibiti hali hiyo, anatarajia kuendesha oparesheni kuanzia Machi 15, mwaka huu.

Pia Mtatiro aliwataka maofisa mapato kusimamia na kufanya ukaguzi kwa wafanyabiashara kama wanatoa stababadhi kwa wajeta wao baada ya kununua bidhaa kutoka kwenye maduka yao na kuchukua hatua kwa wafanyabiashara ambao watabainika kutotoa stakabadhi sahihi kwa wateja wao.

HABARI KITAIFA

# Nzige waleta hofu kwa wananchi Longido

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

MAKUNDI ya Nzige yaliyovamia vijiji vilivyopo Kata ya Kimokouwa katika Wilaya ya Longido mkoani Arusha, yameanza kuleta hofu ya baa la njaa na kusababisha hasara kwa wakulima waliopanda mazao ya chakula na biashara karibu na mpaka wa Namanga.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alithibitisha kuwapo kwa makundi Nzige kuhama vijiji kwa vijiji kuelekea mpakani na wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro.

"Nzige walionekana kwa mara ya kwanza juzi jioni katika mpaka wa Namanga unaozitenganisha nchi za Kenya na Tanzania, wameshaingia Kijiji cha Eworendeke na Kimokouwa vilivyopo Kata ya Kimokouwa, Wilaya yetu ya Longido," alisema na kuongeza:

"Wameshaanza kula majani na matawi ya miti, lakini kuvamia maeneo ya kilimo bado sijapata taarifa za uharibifu isipokuwa wakulima wengi wa Wilaya yetu wapo ukanda wa West Kilimanjaro (Siha),"alibainisha.

"Kwa sasa wameingia eneo la wanyamapori , tumeshawasiliana na wataalamu wa Wizara ya Kilimo nao wamesema wanawasiliana na wataalamu wao wa Kanda ya Kaskazini. Hivyo muda si mfupi tutapata msaada."

Akizungumzia uvamizi wa Nzige hao, Diwani wa Kata ya Kimokouwa, Solomon Kool, alisema hivi sasa pia jamii za wafugaji nazo zinahofia kupotea kwa maeneo ya malisho kutokana na kundi la nzige hao.

"Nzige hawa walitokea eneo la Orkong'u upande wa mpaka wa Kenya kuingia Tanzania. Wamegawanyika katika makundi mawili, kuna kundi lililoelekea upande wa Sinya, Tarafa ya Enduiment na lingine ndiyo hili lilikobaki hapa Kitongoji cha Sikarida " alifafanua Kool.

Kwa mujibu wa Kool, kundi kubwa la nzige lilivamia Kijiji cha Eworendeke na kushambulia zaidi ya hekari 40 za malisho ya mifugo.

Alisema wakazi wa kata hiyo asilimia 95 wanajishughulisha na ufugaji na uhifadhi huku asilimia tano akijishughulisha na kilimo cha mahindi, magharage, nyanya na vitungu.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Eworendeke, Lomayan Ole Sambau, alisema ameshafanya mawasiliano na vijiji vinavyopakana na kitongoji hicho ili nzige hao wanapooneka watoe taarifa na kupata msaada wa kudhibitiwa.

"Hawa Nzige wana safiri umbali mrefu zaidi ya kilomita 70, hivyo tumewaeleza watu wa Kimwati na Sinoniki, Tarafa ya Engarenaibor wakiwaona watoe taarifa," alidai Ole Sambau.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Dk. Gerald Kusaya alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu uvamizi hao nzige hao alisema:

"Lipo kundi la wadudu aina ya Nzige zaidi ya Milioni 50 walioingia nchini kupitia Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro na baadaye kuelekea baadhi ya maeneo ya vijiji vya Wilaya ya Same na Simanjiro, mkoani Manyara.

Aidha, Dk. Kusaya alisema Nzige hao waliingia nchini kupitia kijiji jirani cha Karambandea kilichopo jirani na mbuga ya wanyamapori ya Tsavo, Kenya.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, akizungumza wakati wa maadhimishoya Siku ya Mwanzilishi wa Skauti Duniani, katika Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Kamishna Mkuu Skauti Tanzania, Grace Kado nakulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Skauti ya Mkoa wa Dar es Salaam, Abdull Abibi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Laini za simu kuwa na neno la siri

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema ifikapo Julai mosi, laini zote zitakazotolewa zitakuwa na neno la siri ambalo mteja atatakiwa kulibadilisha ili kutumia laini mpya yenye usalama.

Kwa mujibu wa ujumbe uliosambazwa jana kwenye simu za wateja mbalimbali ambao ulithibitishwa na Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TCRA, Semu Mwakyanjala, utaratibu huo utalinda wateja.

Alisema utaratibu huo una lengo la kuwalinda wananchi kwenye matumizi ya mawasiliano.

"Laini inapopotea ikachukuliwa na mwingine anaitumia vibaya lakini kwa kuwa na neno la siri, itamlinda mtumiaji na kuondokana na utumiaji usio salama,"alisema.

Mwakyanjala alisema utaratibu huo ni kwa mujibu wa sheria ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 na kanuni zake za 2018.

"Tunataka matumizi bora ya mifumo ya simu si kwa ajili ya kuongea bali kama benki, hivyo usalama ni muhimu kwa ajili ya kuwalinda watumiaji, watu watumie simu kwa biashara na maendeleo kuliko kufanya uhalifu,"alisema.


Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

**INVITATION TO TENDER – TIME EXTENSION**
**TENDER No. TNRF/BMZ/ 2-6/02/2021**
**CONSTRUCTION WMAs OFFICES, RANGER POST, RENOVATION OF TOURIST HOSTEL AND INFORMATION CENTRE**

**1. Background**

The Tanzania Natural Resource Forum (TNRF) is a network organization registered in 2006 as a Non-Governmental Organization (NGO), with the aim of promoting the improvement of natural resource governance to achieve more sustainable rural livelihoods and better conservation outcomes. TNRF works for improved natural resources governance by helping to bridge the gap between:

a) People's local natural resource management needs and practices, and
b) National natural resource management priorities, policies, laws and programs

TNRF has received funding from the Federal Ministry for Economic Cooperation and Development (BMZ) through World Wide Fund for Nature (WWF) Tanzania Country Office to implement some of activities within Climate change adaptation support for community managed areas (CBNRM) project aiming at supporting Protection of key ecosystems, increased resilience and adaptation for sustainable use by local communities. To strategically support operations of both Enduimet and MAKAO WMAs, improved infrastructure is very key to address the challenges they are facing like human wildlife conflicts, poaching and diminished income flow to sustain the operations of the WMAs in the light of COVID 19 and climate changes challenges.

**TNRF thus invite interested bidders for the following:**

**Lot 1:** Tender Code TNRF/BMZ/2/02/2021 Construction of office block for MAKAO WMA at Mwangudo, Meatu district

**Lot 2:** Tender Code TNRF/BMZ/3/02/2021 Construction of two observation towers/ranger posts for MAKAO WMA; one at SAPA and second at Shugushi site, Meatu district

**Lot 3:** Tender Code TNRF/BMZ/4/02/2021 Construction of office block for Enduimet WMA at Tingatinga, Longido District.

**Lot 4:** Tender Code TNRF/BMZ/5/02/2021 Construction of information center for Enduimet WMA at Tingatinga, Longido District

**Lot 5:** Tender Code TNRF/BMZ/6/02/2021 Renovation of tourist hostel for Enduimet WMA at Olmolog, Longido district

Interested suppliers/firms may purchase tendering documents from TNRF offices, Plot # 10, Corridor Area, Arusha or via email: info@tnrf.org upon presentation of a request letter duly stating the company name and original bank slip/scanned for Tzs 100,000 (One Hundred Thousand Tanzanian shillings only) for each of the Lots mentioned above being a non- refundable fee. See our bank accounts details below:

**Accounts Name:** Tanzania Natural Resource Forum
**Account No:** 002 – 4002411.
**Bank Name:** Absa Bank (T) Ltd, Arusha Branch

All tenders in one original and one copy, properly filled and enclosed in plain sealed envelopes (Not indicating bidder's name) stating clearly TENDER FOR GOODS, SERVICE AND WORKS should be addressed to:

**Procurement Tender Committee Tanzania Natural Resource Forum P.O BOX 15605,**
**Tel: +255747158888**
**ARUSHA-Tanzania**
**TENDER No. TNRF/BMZ/2/02/2021**

Deposited at the reception of Tanzania Natural Resource Forum Offices, Plot # 10, Corridor
Area, Arusha.
**Deadline for application is 1st March, 2021 at 11am**

# LHRC yaingilia kati sakata la mwanafunzi aliyetoroshwa

Na Thobias Mwanakatwe

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimeingilia sakata la mwanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari Itope anayedaiwa kutoroshwa na mfanyabiashara wa Kyela mkoani Mbeya, ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Mfanyabiashara anayetuhumiwa kufanya tukio hilo Desemba 29, mwaka jana, lakini hajakamatwa kwa takribani miezi miwili sasa licha ya tukio hilo kuripotiwa polisi na mzazi wa mwanafunzi huyo ambaye hajulikani aliko hadi sasa.

Kutokana na hali hiyo, juzi LHRC ilituma wanasheria wake kwenda wilayani Kyela ambako walizungumza na mzazi wa mwanafunzi na walimu wa shule anayosoma mwanafunzi huyo, ili baada ya hapo hatua za kisheria zichukuliwe.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, akizungumza na gazeti hili jana, alisema wakiwa wasimamizi wa sheria na haki za binadamu, wameona wasaidie kufuatilia suala hilo ili haki itendeke.

"Tumetuma wanasheria wetu wafuatilie suala hili kwa kina na baada ya hapo tutaangalia namna ya kusaidia kuchukua hatua kisheria, " alisema.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Simon Mwasitu, alisema amefurahishwa na ujio wanasheria wa LHRC na kwamba sasa ana uhakika suala hilo haki inakwenda kutendeka.

Alisema amekuwa na mawazo kila siku kwasababu ni takribani miezi miwili sasa hajui mtoto wake yuko wapi na kama yupo salama na kwamba kila mara amekuwa akienda kituo cha polisi Kyela mjini kuulizia kama mtuhumiwa amepatikana lakini hakuna mafanikio yoyote.

Mara ya kwanza tukio hilo liliporipotiwa polisi, mfanyabiashara huyo alifunguliwa jalada namba KY4IR/07/2021 katika kituo cha Polisi Kyela.

Alisema mara ya kwanza alitoa taarifa kuwa mtoto wake alitoroshwa na mfanyabiashara huyo tangu Desemba 29, 2020 saa 1:30 usiku na kumpeleka kwenye moja ya hoteli za kitalii Matema Beach.

**Kutoroshwa kwa mwanafunzi huyo kumewashtua na kuzua hofu kubwa kwa wananchi wa mji wa Kyela ambao wanahoji ni kwanini mfanyabiashara huyo hakamatwi na anaendelea na matukio haya huku miradi yake aliyoiwekeza Kyela ikiendelea kama kawaida.**

Mwasitu alisema ilipofika Desemba 30, 2020, mfanyabiashara huyo alimtuma rafiki yake wa karibu (anamtaja jina) kwenda kuonana na wazazi wa mwanafunzi huyo.

"Rafiki wa mfanyabiashara huyo alipokuja kwangu kuniona alinieleza kuwa ametumwa na mfanyabiashara huyo kwamba tusimtafute Mwanafunzi yuko naye na kwamba anaomba amuoe kabisa na yuko tayari kutoa hela atakayohitaji," alisema.

Mwasitu alisema wao kama wazazi walikataa ombi la mfanyabiashara huyo kutaka amuoa mtoto wao kinyume na sheria za nchi, badala yake walimweleza aliyetuma akamwambie kuwa amrejeshe nyumbani mwanafunzi huyo na baada ya kurudi watampima hospitali kuona kama yuko salama na kama atakuwa salama hawatahitaji kuendelea na mambo ya kesi.

Siku tisa baadaye wakati Jeshi la Polisi likiiendelea kumsaka mfanyabiashara huyo, mwanafunzi huyo alirejeshwa nyumba kwao kwa kupakizwa kwenye basi kutokea Dar es Salaam na mfanyabiashara huyo ambapo binti huyo alikwenda polisi kutoa maelezo polisi kuthibitisha kwamba alikuwa na mfanyabiashara huyo.

Baada ya kutoa maelezo polisi alipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela kupimwa ambapo kulingana na maelezo ya baba Mzazi aliyoelezwa na daktari ilithibitika kuwa mwanafunzi huyo alibakwa.

Kutoroshwa kwa mwanafunzi huyo kumewashtua na kuzua hofu kubwa kwa wananchi wa mji wa Kyela ambao wanahoji ni kwanini mfanyabiashara huyo hakamatwi na anaendelea na matukio haya huku miradi yake aliyoiwekeza Kyela ikiendelea kama kawaida.

Walisema mfano ana ujenzi wa nyumba Kyela unaendelea kama kawaida na muda wote mafundi wake wanachapa kazi na simu zake za mkononi muda wote zinapatikana.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakichimba mtaro kwa ajili ya kulaza bomba la inchi mbili na nne kwa umbali wa kilomita tatu, ili kupeleka huduma ya maji katika nyumba za watumishi wa Halmashauri ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkutano mkubwa madini kuanza Dar

Na Joseph Mwendapole

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, leo anatarajiwa kufungua mkutano mkubwa wa kimataifa wa sekta ya madini utakaoambatana na maonyesho ya bidhaa za madini jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema nchi tisa zimethibitisha kushiriki mkutano huo utakaofanyika kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC).

Alisema lengo la mkutano huo ni kuhamasisha Watanzania wengi zaidi kuingia kwenye sekta ya madini na kupata maoni ya namna ya kuboresha sekta hiyo.

Biteko alisema serikali imeandaa mkutano huo kwa lengo la kujua changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara wa kwenye sekta ya madini na kuzitafutia majibu.

Alisema mkutano huo wa siku tatu unafuatia ule uliofanyika baina ya Rais John Magufuli na wafanyabiashara hao ambapo Rais alitoa maelekezo kadhaa ya kuboresha sekta hiyo.

Sekta hiyo, alisema kwa asililimia kubwa inafanywa na watu binafsi na serikali ni msimamizi tu hivyo imeona umuhimu wa kukaa meza moja na kujadili namna ya kusonga mbele.

"Tunataka kupata maoni ya wafanyabiashara wa sekta binafsi kwa sababu kama mnavyojua sekta hii inamilikiwa kwa asilimia kubwa na watu binafsi, tunataka watuambie changamoto tuzitatua twende mbele," alisema.

Biteko alisema Tanzania imekuwa ikialikwa kwenye nchi mbalimbali kwenye mikutano ya kujadili namna ya kuboresha sekta ya madini lakini safari hii imeona iandae na kuzialika nchi hizo.

Alisema pembeni ya mkutano huo kutakuwa na maonyesho mbalimbali ya madini ambapo wachimbaji na kampuni za madini watakuwa wakielimisha wananchi kuhusu sekta hiyo.

Biteko alisema mkutano huo ni muhimu kwani utawakutanisha wadau wa viwanda na wafanyabiashara wa madini na kubadilishana uzoefu na ujuzi wa huduma wanazotoa.

"Sekta hii ni pana kuna wenye viwanda, watoa huduma za chakula, mitambo na huduma zingine ambao watashiriki mkutano huu hivyo tutautumia mkutano huu kuiambia dunia kwamba Tanzania ni sehemu sahihi ya kuwekeza hasa sekta ya madini," alisema.

Biteko alisema serikali imejitahidi kuwadhibiti matapeli wa madini ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakiwasumbua wawekezaji wanaokuja kuuza au kununua madini.

Waziri Biteko alisema kwenye mkutano huo kutatolewa tuzo mbalimbali kwa wadau waliofanya vizuri zaidi kwenye sekta hiyo ikiwemo walipa kodi wazuri na kampuni ziliyofanya vizuri kwenye utoaji wa huduma kwa jamii.

Biteko alisema serikali imejitahidi kutatua baadhi ya changamoto zilizokuwa zikiwakabili wafanyabiashara wa madini kama vile kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi zingine ambazo walikuwa wakizilalamikia.

Alisema serikali imejitahidi pia kuweka mazingira mazuri ili madini yaongezewe thamani hapa hapa nchini badala ya kusafirishwa nje ya nchi yakiwa ghafi.

## HABARI KITAIFA

# Wabunge walilia barabara kuepusha vifo vya wajawazito

**Na Alphonce Kabilondo, Geita**

UBOVU wa miundombinu ya barabara kwenye baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe na Bukombe mkoani Geita, zimeelezwa kuchangia vifo vya kinamama wajawazito kutokana na kushindwa kufika kwenye vituo vya afya kwa wakati.

Malalamiko hayo yametolewa jana na Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, Nicodemus Maganga pamoja na Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Geita, Rose Busiga wakati wa kikao maalumu cha majadiliano ya maendeleo ya barabara ya Mkoa wa Geita.

Mbunge Maganga alisema hali ya miundombinu ya barabara kwenye kata zote 17 za Wilaya ya Mbogwe siyo rafiki kwa muda mrefu hasa ndani ya kipindi cha miaka miwili hadi sasa.

Pia, Mbunge huyo alisema kuwa barabara zenye changamoto kubwa ni kutoka vijiji vya Budoda na Ngema kuelekea Masumbwe mjini ambazo zimekuwa kikwazo kwa wananchi wa vijiji hivyo hasa kina wajawazito.

"Kutoka Budoda kwenda Masumbwe kuna mto, wajawazito wanapofika mtoni, kuna watu wanaowavusha kwa mitumbwi, wamekuwa wakijaribu kupanda ile mitumbwi wakati mwingine kuna upepo, mitumbwi inashindwa kuvuka wanaishia kuzama. "Tayari Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) kuna daraja waliweka, lakini halijaanza kufanya kazi, na ujenzi una miaka miwili sasa, jimbo langu kwenye kata nyingi kuna wakulima wa matiki maji, mahindi na ndengu, mpaka sasa wameshindwa kusafirisha mazao yao," alisema Maganga.

Akichangia wakati wa kikao hicho, Mbunge Viti Maalumu Mkoa wa Geita, Busiga alisema kuwa barabara ya kutoka Bukombe kuelekea Katoro-Geita barabara ni mbovu ambayo imefanya kina mama wengi wanaoenda kujifungulia hospitali ya rufaa Geita kushindwa kufika kwa wakati na kupelekea vifo vya wajawazito.

"Mimi kama mwakilishi wa wanawake, barabara hii ikitengenezwa, wamama wote watashukuru sana serikali yao, maana wamekuwa wakilalamikia kwa muda mrefu sana, naiomba TANROADS watengeneze hii barabara ili wasaidie wajawazito waweze kufika kwa haraka," alisema Rose.

Naye, Meneja wa TANROADS Mkoa wa Geita, Mhandisi Harun Senkunku, alisema wametenga takribani Sh. Bilioni 13.08 kwa ajili ya ukarabati wa barabara huku Meneja TARURA Mkoa wa Geita, Mhandisi Chacha Moset alisema taasisi hiyo imepanga kutumia bajeti ya Sh. Milioni 800 ili kufanyia ukarabati maeneo yenye changamoto ya miundombinu ya barabara zilizo chini ya mamlaka hiyo mkoani hapa ikiwamo Mbogwe na Bukombe.



Kaimu Mkuu wa kitengo cha Uandaaji wa Viwango vya Bidhaa za Mitambo wa Shirika la Viwango nchini (TBS), Mhandisi Arnold Mato, akitoa mada wakati wa mafunzo kuhusu viwango na matakwa ya viwango kwa wazalishaji, waagizaji na wasambazaji wa mabati na koili za mabati hapa nchini, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RUWASA Ruvuma yadhamiria kumaliza kero ya maji vijijini

**Na mwandishi Wetu, SONGEA**

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Ruvuma, imejipanga kuhakikisha matatizo ya huduma hiyo kwa wananchi wa mkoa huo yanakuwa historia ndani ya muda mfupi ujao.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Rebman Gansonga, alibainisha hayo juzi alipokuwa akielezea mipango ya kumaliza kero ya huduma na utekelezaji wa miradi ya maji na mwelekeo wa wakala katika utoaji huduma vijijini.

Mhandisi Ganshonga alisema hali ya upatikanaji huduma ya maji kwa kila Halmashauri hadi Juni, 2019 ilikuwa ikipatikana kwa asilimia 61 ya watu katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea yenye watu 141,427 ambao ni watu 86,270.

Kwa sasa alisema halmashauri hiyo ina vituo vinavyotoa maji 951 kati ya hivyo vinavyofanya kazi ni vituo 590.

Kwa mujibu wa meneja huyo, katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, RUWASA inahudumia wakazi 90,730 na kwamba watu wanaopata huduma ni 45,479 sawa na asilimia 50. Huku kukiwa na vituo vya kutolea maji ni 401 kati ya hivyo vituo vinavyofanya kazi ni 372.

"Katika Halmashauri ya Mbinga yenye watu 235,648, watu wanaopata maji ni 123,648 sawa na asilimia 52.4 na idadi ya vituo vya kuchotea maji ni 375, vituo vinavyofanya kazi ni 196," alisema.

Meneja huyo pia alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo yenye wakazi 226,945, wanaopata huduma ya maji ni 147,515 sawa na asilimia 65. Alisema wilaya hiyo ina vituo 939 vya kuchotea maji huku vinavyofanya kazi vikiwa 484.

Alibainisha zaidi kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru yenye wakazi 256,510, wanaopata huduma ya maji ni 164,166 (asilimia 64) na kwamba vimejengwa vituo vya kuchotea maji 954 wakati vinavyofanya kazi ni 714.

Kwa mujibu wa Meneja huyo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa yenye wakazi 146,160, watu wanaopata huduma ya maji ni 73,080 ambao ni asilimia 50.0 na kwamba vituo vya kuchotea maji ni 645 wakati vinavyofanya kazi ni 312.

"Katika Halmashauri ya Madaba yenye wakazi 53,883, watu wanaopata huduma ya maji ni 33,407 sawa na asilimia 62.0 na ina vituo vya kuchotea maji 419 huku vinavyotoa maji ni 267," alisema.

Mhandisi Ganshonga alisema katika Halmashauri ya Mbinga Mji yenye wakazi 68,338, watu wanaopata maji ni 32,500 sawa na asilimia 47.7 na kwamba katika halmashauri hiyo kuna vituo 305 vya kuchotea maji na kati ya hivyo vituo vinavyofanya kazi ni 130.

"Kwa ujumla katika mkoa wa Ruvuma, RUWASA inahudumia wakazi 1,219,642 na kati ya hao, wanaopata maji ni 704,065 sawa na asilimia 57.9. jumla ya vituo vya kuchotea maji ni 4,989 na vinavyofanya kazi ni 3065'," alibainisha.

Hata hivyo, alisema hali ya upatikanaji wa maji katika halmashauri zote nane mkoani Ruvuma hadi Desemba, mwaka jana, ilikuwa kwa wakazi 833,361 kati ya 1,344,397 kupata maji sawa na asilimia 62.6. Pia alisema bajeti ya RUWASA Ruvuma katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 imelenga kutekeleza miradi ya maji 77 katika Wilaya za Songea, Mbinga, Namtumbo, Tunduru na Nyasa na Sh. 17,095,079,568.15 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

# Majaliwa kubariki kilele cha Majimaji

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri Mkuu, Kassmu Majaliwa, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika Kilele cha Maadhimisho ya Kumbukizi ya Vita Vya Majimaji na Tamasha la Utalii wa Utamaduni linalotarajiwa kufanyika Songea, Ruvuma kuanzia Februari 25, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Noel Lwoga, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa tamasha hilo lililoandaliwa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Baraza la Mila na Desturi la Mkoa wa Ruvuma na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Alisema tamasha hilo litazinduliwa rasmi na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro na kwamba kilele ni Februari 27 na kwamba wageni mbalimbali kutoka Malawi na Zambia wanatarajiwa kuhudhuria.

Dk. Lwoga alisema malengo ya maadhimisho hayo ambayo hufanyika kila mwaka, ni kuwakumbuka mashujaa waliopigana vita vya Majimaji na kufa wakitetea maslahi mapana ya taifa wakiwamo mashujaa 67 walionyongwa na wakoloni mjini Songea Februari 27, 1906 na kuzikwa katika makaburi Makumbusho ya Majimaji.

"Tamasha linalenga katika kutoa fursa kwa wananchi wa Tanzania kuenzi, kutunza na kuendeleza urithi wa utamaduni na wa asili kwa ajili ya kizazi cha sasa na vijavyo," alisema Dk. Lwoga.

Tamasha hilo linalenga katika kuthamini mchango wa wazee na viongozi waliotangulia akiwamo marehemu Dk. Lawrence Gama, katika kuleta maendeleo ya mkoa wa Ruvuma na ukanda wa Nyanda za Juu Kusini kwa ujumla.

Dk. Lwoga aliongeza kuwa maadhimisho haya ni moja ya mikakati ya serikali ya kutangaza na kukuza utalii wa malikale na utamaduni kwa kutumia matamasha.

Amesema ili kuenzi wazee hao, kaulimbiu ya maadhimisho mwaka huu ni "Maisha ya Wazee Wetu, Fahari Yetu.

Aidha, Dk. Lwoga alisema maadhimisho hayo yataambatana na programu mbalimbali kielimu shuleni na maeneo ya wazi pamoja na maonyesho ya wajasiriamali na taasisi mbalimbali za serikali na binafsi zenye lengo la kuelimisha jamii kuhusu historia ya Tanzania na kuhamasisha jamii kutumia na kurithisha urithi kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila mtu azingatie maelekezo kujikinga na madhara kiafya

KATIKA siku za karibuni, kumekuwa na taarifa za vifo vya watu mbalimbali wakiwamo viongozi na mashuhuri, huku wengine wakipoteza maisha baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Sababu kuhusu baadhi ya vifo hivyo, ni matatizo ya kupumua huku wataalamu wa afya wakibainisha kuwa miongoni mwa matukio hayo ni wahusika kutokufikishwa mapema katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Licha ya vifo hivyo ambavyo baadhi ya dalili zinafanana na ugonjwa wa homa ya mapafu, baadhi ya watu wamekuwa wakiilalamikia serikali kuwa haijachukua hatua stahiki katika kupambana na tatizo hilo. Baadhi walivuka mipaka kwamba serikali haijatangaza watu kuchukua tahadhari ikiwamo kujikinga na tatizo hilo.

Hata hivyo, Rais John Magufuli, akiongoza kuagwa kwa mwili ya aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, alivunja ukimya na kuwataka Watanzania kujikinga na maradhi mbalimbali yakiwamo yale yanayoisumbua dunia kwa sasa. Mbali na kujikinga, alisisitiza msimamo wake wa wananchi kuendelea kumwomba Mungu ili aiepushe nchi na majanga yakiwamo maradhi ambayo yanasababisha vifo.

Kama vile haitoshi, Waziri Mkuu naye aliweka bayana jana wakati wa ibada ya mazishi ya Balozi Kijazi, Korogwe mkoani Tanga kwamba serikali haijazuia watu kuvaa barakoa na kuchukua hatua zingine katika kujikinga na maradhi.

Kauli hiyo ya Waziri Mkuu, ambaye ni mtendaji mkuu wa serikali, ilionyesha wazi kwamba serikali inawajali wananchi wake na kuwataka kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na majanga.

Kauli hiyo pia imewapuuza baadhi ya watu ambao wamekuwa wakitaka kujipatia umaarufu kupitia matukio au mambo yanayojitokeza katika jamii na kuitupia lawama serikali kwamba haijafanya kitu au kuchukua hatua zinazostahili.

Watanzania wanapaswa kutambua kwamba suala la kujikinga na maradhi au hatari mbalimbali si lazima litolewe tamko au amri na serikali. Kila mtu anapaswa kila wakati kujilinda.

Kusema kwamba serikali lazima ichukue hatua kwa kila jambo ni sawa na mtu kutaka kukumbushwa hata kujikinga na mbu kupambana na malaria wakati ni suala ambalo mtu anapaswa kuangalia hali halisi ya mazingira katika eneo analoishi.

Kwa mantiki hiyo, kutokana na mfululizo wa majanga yanayoendelea katika jamii hasa na kama alivyotangaza Waziri Mkuu, kila mtu anapaswa kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka pamoja na vitakasa mikono (sanitizer).

Aidha, kama ambavyo tumeshuhudia watu wakijazana katika mikusanyiko mbalimbali bila kuchukua tahadhari, ni vyema wananchi wakachukua tahadhari ikiwamo kuepuka mikusanyiko au kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu mmoja na mwingine.

Tahadhari hiyo pia inatakiwa kuchukuliwa katika maeneo ambayo yana watu wengi kama vile sokoni, vituo vya mabasi, nyumba za ibada na kwenye vyombo vya usafiri ambako wana wanajazana kupita kiasi.

Ni wazi kwamba kama kila mtu atachukua tahadhari na kufuata maagizo ya wataalamu wa afya, ni hakika matatizo ya kiafya yanayoendelea kwa sasa yatapungua kwa kiasi kikubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Sabato Kasika

# Kila mmoja anawajibika kutoa taarifa uharibifu wa miradi ya maendeleo

SERIKALI imeweka umuhimu wa kwanza katika masuala ya utawala bora katika ngazi zote za uongozi, kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za maendeleo na hata zinazohusu hujuma kwa mali za umma.

Hapa wananchi wanahusika kikamilifu kuanzia utunzaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao, na hata kutoa taarifa kwa mamlaka husika anapoona miradi inahujumiwa.

Hivyo ndivyo ambavyo wanatakiwa kufanya, ili miradi hiyo iweze kuwanufaisha wao na vizazi vyao, kwa hiyo hawatakiwi kufanya hujuma ama kuona baadhi ya watu wakihujumu huku wao wakiwa kimya.

Lakini bahati mbaya, baadhi yao hawatambui jukumu hilo na wanadhani kwamba hawawajibiki kutunza na kulinda miradi hiyo katika maeneo yao, na wako tayari kuona ikihujumiwa bila kutoa taarifa. Katika mazingira ya aina hiyo, kuna uwezekano wa miradi mingi kuendelea kuharibika ama kuharibiwa, huku wakishuhudia bila kuchukua hatua kana kwamba si wajibu wao kufanya hivyo.

Bomba la maji linaweza kupasuka na kusababisha yamwagike na kusambaa mitaa na kupotea bure, badala ya watu wa maeneo husika kutoa taarifa, ili mafundi wafike kumaliza tatizo, wanakaa kimya.

Watu huwa ni wa kwanza kubeba ndoo nyingi kwenda kukinga maji yanayomwagika, huku wakidai kwamba wakitoa taarifa watayakosa, hivyo ni bora wawe kimya, ili waendelee kufaidi.

Kitendo hicho kinasababisha upotevu mkubwa wa maji na kuinyima serikali mapato, hivyo ni vyema jamii ikatambua kuwa inatakiwa kutoa taarifa inapoona hali kama hiyo ama hujuma yoyote.

Wauza maji mitaani, nao ni wafaidika wakubwa na inawawia vigumu kutoa taarifa, kwa vile wanajua wakifanya hivyo watayakosa, na kujikuta hawapati fedha zinazotokana na maji, ambayo hawakuyalipia.

Matukio ya aina hiyo yamekuwa yakijitokeza katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam baada ya mabomba kupasuka, ambapo huwa ni kama sherehe, kutokana na watu kukusanya ndoo na kwenda kukinga maji.

Kwa hali kama hiyo, inawezekana wapo baadhi ambao wako tayari kuharibu miundombinu mbalimbali ili wapate vya bure, hali ambayo inaweza kuwakatisha tamaa hata wafadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ninaamini kwamba maelekezo kuhusu la utoaji taarifa kwa mamlaka husika pale miundombonu inapoharibika ama kuharibiwa siyo mageni masikioni mwa Watanzania, lakini inashangaza kwa nini wamekuwa wagumu.

Umefika wakati sasa wananchi kutambua kuwa wana wajibu wa kulinda miundombinu mbalimbali kwenye maeneo yao na pale zinapotokea hujuma, watoe taarifa kwa mamlaka husika badala ya kukaa kimya.

Uharibifu wa miundombonu ama miradi ya maendeleo usigeuke kuwa faida kwao na kuacha kutoa taarifa kwa mamlaka husika, wajue kuwa ni hasara kwao iwapo wataendelea kunyamaza.

Mfano katika taarifa ya hali ya utoaji huduma ya majisafi na uondoaji taka na mipango ya Mkoa wa Dar es Salaam iliyowahi kutolewa na serikali miaka ya nyuma, ilionyesha matatizo mbalimbali katika utoaji wa huduma hiyo muhimu.

Miongoni mwake ikiwa ni wizi wa maji, uharibifu na wizi wa miundombinu ya majisafi na majitaka na kuchangia kwa kiasi kikubwa cha maji yasiyolipiwa zaidi ya asilimia 45.

Ni kweli kwamba jiji la Dar es Salaam lina changamoto ya kutopatikana kwa maji ya kutosha yanayokidhi wingi wa wakazi wake, lakini hilo lisiwe sababu ya kuruhusu uharibifu wa miundombinu.

Kuna miradi miundombinu mingi ya maendeleo, lakini hiyo ya maji imekuwa ikionewa zaidi, kufuatia wananchi kunyamaza kimya pale wanapooona bomba limepasuka na kumwaga maji mitaani.

Hawaoni kwamba ni hasara kwao, badala yake inageuka kuwa neema, ambayo mwisho wa siku wanaweza kujikuta wakikosa huduma hiyo muhimu, kwa sababu ya uzembe au makusudi.

Wakati wakifanya hivyo kwenye maji, linapotokea tatizo la kukatika ama uharibifu wa miundombinu ya umeme huwa ni wepesi wa kulalamika pale mafundi wanapochelewa kufika kufanya marekebisho.

Kwenye suala la maji, hata mafundi wasipofika kurekebisha tatizo, wanaona ni jambo la kawaida, kwa vile wanajichotea bure, lakini linapotokea tatizo kukatika kwa umeme kwa siku moja tu malalamiko yanakuwa ni mengi.

Utasikia wakidai kwamba wametoa taarifa tangu siku fulani, lakini bado mafundi hawajafika, lakini hatua hizo za kutoa taarifa hazifanyiki pale linapotokea tatizo la kupasuka kwa bomba la maji.

Wananchi kunyamazia uharibifu wa miundombinu ya maendeleo ni sawa na kujikwamishia maendeleo yao wenyewe, hivyo ni vyema wakabadilika na kuchukua hatua zinazostahili.

## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Tuzalishe wabunifu na si wasaka ajira



Nkwazi Mhango, Canada

HIVI karibuni, kulikuwa na mjadala mkali bungeni juu ya wasomi tuzalishao siku hizi kutoweza kuwa na ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa. Tukiachana na kujisahaulisha, kipi kilichobadilika kwenye mfumo wetu wa elimu tangu kupata uhuru?

Je, hawa wanaolalamika si matunda ya mfumo huu huu ambao walishindwa kuubadili? Je nini kifanyike? Je, tuanzie wapi na lini kuzalisha wale kwa kimombo naweza kuita thinkers and inventors but not job seekers, yaani wenye kufikiri sawa sawa na wawekezaji na si wasaka ajira.

Katika kujaribu kutoa mapendekezo juu ya namna ya kubadili mfumo wetu, nilisikia baadhi ya wabunge, hasa wale waliokata tamaa na kushindwa kubuni mbinu mbadala, wakipendekeza kuwa tupunguze usajili wa vyuo vinginevyo watakaotaka kuvisajili watuhakikishie ajira. Hii ililenga kuandaa watu ambao tayari vyuo vitakuwa vimeishawatafutia kazi. Je, hili ni endelevu?

Kwanza, kazi ya vyuo si kuwatafutia watu ajira bali kuwapa elimu waliyoridhika nayo hadi wakaomba kujiunga na vyuo husika. Vyuo haviwaiti watu kuja kusoma bali watu huomba viwapokee na kuwaelimisha. Pili, si lazima kila huduma imhakikishie mafanikio kila anayoipata toka kwa anayoitoa. Vyuo si sawa na majiko au hoteli. Hutoa ujuzi unaoweza kumfaa mtu maisha yake.

Wengine wangependekeza hili la kuwatafutia wahitimu wa vyuo kazi lakini si wabunge. Wao wabunge wanatuhakikishia nini tunapowachagua? Ni wangapi wamekaa bungeni makumi ya miaka bila kuleta mabadiliko kwenye majimbo yao? Kwa nini hawapitishwi kwa kutuhakikishia watatimiza ahadi na malengo ya kuchaguliwa kwao? Mfumo wa kuzalisha wasaka ajira utaweza kujibadili kirahisi bila kuwapo na ving'ang'anizi? Kuubadili, tunahitaji mawazo yenye siha na si ya kukata tamaa au kufikiri juu ya visivyofikirika.

Je, madaktari ambao wagonjwa wao watakufa nao wafukuzwe kazi au walimu ambao wanafunzi wao watashindwa? Je, polisi ambao maeneo yao yatakumbwa na uhalifu itakuwaje?

Nadhani badala ya kuanza kulaumu kifaa, tuanze kufikiri. Hata hivyo, sishangai wanaotoa mapendekezo kama haya ya kichovu. Wengi wao si wasomi, wanachukia usomi na wasomi, kama baadhi yao walivyoonyesha kwenye michango yao na hawapendi hata kujiendeleza mbali na kuchukia wasomi. Wapo waliosikika wakisema kuwa watu wenye PhD au shahada nyingine za vyuo wasiajiriwe kwa vile wamewaangusha. Je, Magufuli naye na PhD yake amewaangusha?

Tuache mjumuisho ambao, kisomi, ni dalili ya uvivu wa kutafiti na kuelewa mambo. Tatizo, kwa mfano, matatizo kama vile majungu, rushwa, uvivu, udokozi, ukosefu wa uzalendo, wizi na mengine kama hayo si ya la wasomi wala vihiyo. Ni tatizo la watu binafsi. Kuna wasomi mafisadi sawa na vihiyo.

Kadhalika kuna vihiyo waadilifu sawa na wasomi. Huwezi kuchukia au kuharamisha utuli eti kwa sababu unasababisha mafua badala yake ukaamua kutumia samadi, pamoja na harufu yake mbaya, eti kwe vile haisababishi mafua. Hapa dawa ni kutafuta namna ya kutumia utuli na kuzuia mafua na siyo vinginevyo.

Swali kuu na la kufikirisha hata kama ni gumu tunalopaswa kujiuliza na kulitafutia jibu sahihi haraka ni kwanini wenzetu waliweza kufanikiwa kwa kutumia wasomi badala ya kuanza kufikiria kwa kurudi nyuma badala ya kwenda mbele.

Tuhitimishe; dawa nyingine ya kuondokana na wasomi au wananchi wezi bila kujalisha usomi wao ni kuwa na nchi yenye mfumo unaohimiza maadili kisheria na kimila. Nimekuwa mpiga kelele mkubwa wa dhana nzima ya kuhakiki mali za watumishi wetu wa umma na watanzania kwa ujumla. Hii, licha ya kutia nidhamu, huleta uwajibikaji na uchumaji wa halali na kupunguza tamaa za mali na wizi vilivyotamalaki nchini kiasi cha watu kusoma au kutosoma ili kutafuta nafasi ya kulihujumu taifa.

Hata hawa wanaopiga kelele kuwa wasomi wameangusha taifa hili, ukiwauliza, pamoja na kujisifia na ukihiyo wao wameifanyia nini nchi zaidi ya hao wanaowalaumu. Kwanza, kutotaka kujielimisha ni dhambi ukiachia mbali kuwa kikwazo cha maendeleo hasa kama dhana nzima ya kusoma ni kumkomboa mwenye kuelimika au kupokea elimu.

Ni kweli. Tunao wasomi wa ovyo walioshindwa kujikomboa wao na jamii yao . Hata hivyo, mateso ya asiyesoma katika maisha ni tofauti na aliyesoma. Elimu, hata isipoleta ajira, humfanya aliye nayo angalau kujiamini akilinganishwa na asiye nayo. Ndiyo maana, watu wanaghushi shahada au kujipatia shahada za vyuo za juu hata kama hawajazisomea. Hii ni kutokana na kutaka wapewe heshima ambayo wenye shahada husika hufaidi au kupewa na jamii.

Mfano, mtu mwenye shahada ya uzamivu (Ph.D), si sawa na tajiri mwenye cheti cha darasa la saba. Asiyejua kusoma na kuandika halingani na asiyejua kusoma na kuandika. Asiyeona ajuaye kusoma na kuandika ni bora kuliko mwenye macho asiye na ujuzi huo.

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mfumo Elimu ya Juu ni jipu



Na Joseph Kulangwa

VIONGOZI duniani katika kufanikisha majukumu yao ya kiongozi, wamejiwekea mifumo na taratibu za faragha na za wazi, za kupokea taarifa kwa siri au kwa kukutana ana kwa ana na wananchi.

Vipo vikosi maalumu ambavyo hupenyeza taarifa kwa kiongozi, lakini pia mbali na vyombo vya habari, viongozi hutumia wasaidizi wao wa chini kupata taarifa hizo.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere. Mbali na kupata taarifa kwa siri, alikuwa na utaratibu wa kuzungumza na wazee wa Dar es Salaam, kila alipokuwa na jambo la kuzungumza na taifa.

Alhaji Ali Hassan Mwinyi, alikuwa na utaratibu wa kusikiliza matatizo ya wananchi katika Ofisi Ndogo ya Makao Makuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mtaa wa Lumumba, Dar es Salaam, huku pia akialika wanahabari Ikulu kila mwisho wa wiki, kuzungumza nao au kupitia mwakilishi wake.

Benjamin Mkapa, alihutubia taifa kila mwisho wa mwezi, utaratibu ambao pia ulirithiwa na Dk. Jakaya Kikwete. Ili mradi kila mmoja kwa njia yake, alipata taarifa alizostahili au kuzitaka.

Dk. John Magufuli, amekuwa akizungumza na taifa katika karibu kila hafla au tukio linalofanyika Ikulu, lakini pia akisimama barabarani akiwa kwenye ziara kutoka au kwenda mkoa fulani nchini. Katika ziara hizo, amekuwa akisikiliza kero mbalimbali za wananchi na kuchukua hatua wakati mwingine za papo hapo.

Hivi karibuni, akiwa katika ziara kama hizo, Rais Magufuli alikutana na kijana Yusufu Juma, aliyedai anatoka Musoma Vijijini, akijitambulisha kuwa amesoma 'Udaktari Engineering', huku akibabaika kueleza kasoma wapi, akidai Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), na alipoulizwa na Rais kiko wapi, akasema Dodoma!

**Ili kuachana naye, Rais alimwambia apeleke vyeti vyake kwa Mkuu wa Wilaya na kuishia hapo. Ni dhahiri, kijana Yule kwa macho ya kawaida, alionekana hakuwa sawa kifikra ndiyo sababu hata aliyokuwa akiyasema haya kuwa na matinki licha ya kukosa hata mtiririko mzuri.**

Na katika hali ya kubabaika zaidi na kuonesha yawezekana kuwa 'mwezi mchanga', akang'ang'ania kuwa amesomea kutengeneza vifaa tiba na kulalamika kuwa wakati yeye ana shahada na hana ajira, wenzake waliomali za darasa la saba wana ajira na kudai anaogopa kuiba, kwani ataishia jela.

Huku Rais akionekana dhahiri kubaini tatizo la kijana huyo, au athari hasi kichwani, alimwuliza kiwango chake cha ufaulu kwa maana ya mitihani yake ya chuo kikuu (GPA), akamjibu alipata 32, na kuamshaki cheko na Rais kuwaambia hadhira kuwa duniani hakuna GPA ya kiwango hicho. Kawaida kiwango cha juu cha GPA ni kati ya 4.4 na 5.0.

Ili kuachana naye, Rais alimwambia apeleke vyeti vyake kwa Mkuu wa Wilaya na kuishia hapo. Ni dhahiri, kijana Yule kwa macho ya kawaida, alionekana hakuwa sawa kifikra ndiyo sababu hata aliyokuwa akiyasema haya kuwa na matinki licha ya kukosa hata mtiririko mzuri.

Pamoja na udhaifu huo, bado alikuwa na ujumbe kwa umma, kwamba kuna tatizo katika ajira kwa vijana hususan wanaomaliza elimu ya juu nchini na kurudi mitaani kutafuta ajira.

Akizungumza bungeni hivi karibuni, Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, aligusia tatizo hilo, akisema mfumo wa mafunzo kwa vijana wa vyuo vikuu nchini, hauwasaidii kupata ajira, na badala yake ni vizuri kuongezwa vyuo vya ufundi, ili kutoa vijana wanaoweza kutumia elimu yao kujiajiri na kuzalisha mali. Bila hivi, linatengenezwa bomu lisilozuilika katika jamii. Alamsiki!

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

# Kwaheri Maalim Seif mwalimu somo la amani

WIKI hii ilikuwa ya majonzi makubwa kwa Watanzania kutokana na kuondokewa na wapendwa wetu wakiwamo viongozi wetu waandamizi ambao walifariki dunia kwa nyakati tofauti.

Miongoni mwa viongozi hao waliotuacha na majonzi makubwa ni pamoja na aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefariki dunia Februari 17, mwaka huu na kuzikwa kijijini kwao, Mtambwe, Kaskazini Pemba siku iliyofuata.

Kiongozi mwingine mwandamizi aliyefariki dunia wiki hii ni Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, ambaye alizikwa jana Korogwe mkoani Tanga.

Hakika viongozi hawa watakumbukwa walivyotoa mchango katika kuleta maendeleo na kudumisha amani katika kipindi cha uhai wao.

Nikianza na Maalim Seif, kifo chake hakika kimeacha majonzi makubwa. Uhakika wa jinsi wananchi walivyopata majonzi unajionyesha maelfu ya wananchi walivyofurika kuuaga mwili wake jijini Dar es Salaam na Mnazi Mmoja, Unguja na kisha uwanja wa Gombani, kisiwani Pemba.

Maelfu ya wananchi walisimama njiani huku nyuso zao zikionyesha majonzi makubwa na baadhi yao kuangusha vilio walipoliona gari lilipopakia jeneza la Maalim Seif huku wengine wakiinamisha vichwa nyao na kuvitikisa kwa ishara ya maumivu makali.

Ukitafakari kwa undani sana kwa nini Maalim Seif amegusa sana mioyo ya Watanzania wengi, utabaini kuwa alikuwa mwalimu wa amani nchini hususani katika visiwa vya Zanzibar.

Maalim Seif aliipenda sana nchi yake, alipenda amani na zaidi ya yote aliishi kwa amani na alikuwa tayari kuwafundisha watu aliofanya nao kazi somo la amani kwa vitendo.

Maalim alikuwa tayari kusamehe baadhi ya mambo ambayo katika hali ya kawaida yasingesameheka, lakini kwa mapenzi yake kwa wananchi na kwa amani ya nchi yake, alilazimika kusamehe na kusonga mbele.

Maalim Seif alikuwa na kifua kipana chenye uwezo wa kutunza mambo yote, mema kwa mabaya.

Kutokana na uwezo wake huo aliojaaliwa, alifanya maridhiano bila kikwazo. Yote hii ilitokana na mahaba yake makubwa kwa wananchi wenzake na zaidi ya yote kwa nchi yake hususani Zanzibar.

Ni mwanasiasa ambaye amefanya mwafaka au maridhiano na kila Rais wa Zanzibar tangu mfumo wa vyama vingi uanze nchini. Huyu ni nguzo ya Zanzibar iliyoridhiana na Zanzibar yenye maridhiano kwa hakika ni Zanzibar yenye maendeleo.

Maalim Seif atakumbukwa kwa kuwa baba wa demokrasia ya vyama vingi nchini; mlezi wa vijana wanaochipukia katika siasa za vyama vingi; muumini mkubwa wa ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

Nichukue fursa hii kumpongeza Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, ambaye katika hotuba yake ya salamu za rambirambi alizungumzia suala la kumuenzi Maalim Seif kwa kuendelea kuitetea Zanzibar.

Kwa jumla, Maalim Seif ameacha somo kubwa kwa wanasiasa kwamba unapokuwa mwanasiasa wa upinzani hupaswi kuwa chanzo cha kuvunjika kwa amani katika nchi.

Maalim Seif katika enzi za uhai wake, mara zote alipogombea nafasi ya urais Zanzibar anapoona ameshindwa anakubali lakini hakuwahi kususa kutoshiriki katika serikali ya umoja wa kitaifa ambalo ni takwa la katiba ya Zanzibar.

Viongozi wa aina ya Maalim Seif ni wachache sana kwani tangu alipoondolewa katika chama tawala na kujiunga na vyama vya upinzani alipitia katika misukosuko mingi lakini somo la amani kwa wazanzibar lilimjaa kichwani na hivyo hakutaka kuwa chanzo cha kuivuruga amani.

Vijana ambao wanachipukia kwenye masuala ya siasa wanapaswa kumuiga Maalim Seif kwa kutambua kuwa siasa siyo uhasama wala njia ya kuvunja amani ya nchi bali iwe fursa ya kuwaleta wananchi pamoja katika kudumisha amani.

***MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI AMANI YA NCHI YETU.***

***Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com***

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

# Kanuni 10 za kukabili migogoro ya ndoa- 2

WANANDOA wengi hawana ufahamu wa namna ya kukabili migogoro ya ndoa pale inapojitokeza katika ndoa zao. Katika toleo lililopita, tulijifunza suala zima la migogoro ya ndoa, faida na athari zake.

Wiki iliyopita, katika sehemu ya kwanza ya makala hii, nilizungumzia namna faida za faida za migogoro ya ndoa ni chache zaidi kuliko athari zake. Lakini kubwa zaidi niligusia kanuni 10 za kukabili migogoro hiyo na nilizungumzia baadhi.

Katika sehemu hii, naendelea kudadavua kanuni zingine katika kukabiliana na migogoro hiyo;-

**Jiepushe kuingilia mazungumzo**

Lugha ya staha, utulivu na usikivu vinahitajika katika mazungumzo. Kila mmoja apate nafasi ya kueleza hisia zake na kutoa ya moyoni mwake kwa namna ambayo inajenga na kuleta utulivu wa mazungumzo.

Kila moja anapaswa kuepuka kuzungumza kwa kupayuka, hasira na maneno ya dhihaka. Ni muhimu kujua namna ya kutawala hisia. Epuka kuingilia mazungumzo pale mwingine anapozungumza, hata kama anachosema hakikufurahishi. Ni muhimu kuvumilia na kujieleza katika kusikiliza mwingine anachosema na kujitathimini katika kile kinachoelezwa juu yako. Kusikiliza huonyesha kujali na kiashiria cha dhamira ya mtu mwenye kutaka suluhu.

**Omba msamaha, samehe na kuachilia**

Kukosa ni kwa kila binadamu. Kama nilivyokwisha kueleza awali, hakuna tatizo katika ndoa lisilochangiwa na mume au mke. Ndiyo maana ya kusema kuwa, mjenzi na mbomoa ndoa huwa ni mwanandoa mwenyewe.

Kwa kuwa hakuna mwanadamu asiyekosea, ni muhimu wanandoa wawe wepesi kuombana msamaha na kusameheana na kusahau yaliyopita. Msamaha huachilia uwepo wa Mungu na baraka katika maisha.

Kuomba msamaha ni sehemu muhimu katika utatuzi wa tatizo. Baada ya msamaha, wanandoa waepuke kurudia makosa. Kurudia makosa yale yale kila mara hukatisha tamaa na kuondoa nguvu ya msamaha, hivyo, huzaa tatizo jingine kubwa zaidi.

Msamaha ni tiba ya nafsi iliyojeruhiwa. Kupona kwa nafsi iliyojeruhiwa ni mchakato. Jinsi wanandoa watakavyochukuliana na kutendeana mema, ndivyo uponyaji utakapokuwa wa haraka na suluhu ya dhati kupatikana.

**Ombea uhusiano wenu**

Matatizo mengine katika ndoa hayamalizwi kwa mazungumzo au vikao, bali mpaka Mungu atakapoingilia kati. Wanandoa wajifunze kumwomba Mungu na kupeleka haja zao kwake ili aweze kuwasaidia. Wanandoa wengi si waombaji, bali walalamishi na wanung'unikaji tu. Kulalamika na kunung'unika hakutatui tatizo, sana sana huongeza ukubwa wa tatizo.

Ni muhimu sana Mungu afungamanishwe na maisha ya wanandoa. Huwezi kumsaidia mwenzako kuelewa Mungu asipohusika.Wanandoa watambue kuwa, bila Mungu uhusiano wao hauwezi kudumu. Wanandoa wanahitaji kuombeana kwa Mungu ili pendo la ndoa lidumu ndani yao.

**Jiepushe**

Si busara kulichukulia kwa uzito kila jambo katika uhusiano, kwani mambo mengine ni madogo sana yasiyohitaji kutiliwa maanani na kupewa sifa ya kuwa tatizo. Mambo mengine ni ya kupuuzia tu. Kadri siku zinavyokwenda hujifuta.

Waingereza wanasema, "Many things are just too small to complain about", kwa tafsiri kwamba, mambo mengi ni madogo madogo sana kiasi kwamba hakuna sababu ya kuyalalamikia. Kwa hiyo, mwanandoa epuka kuwa mlalamishi uliyepitiliza. Kama kuna jambo hulielewi, zungumza na mwenzako kwa upendo na upole ili myajenge.

**Tafuta ushauri kwa watu sahihi**

Si busara kukurupuka na kufanya uamuzi utakakuangamiza. Kama kuna tatizo kubwa, ambalo wanandoa mmeshindwa kulitatua, inashauriwa kutafuta ushauri kwa watu waaminifu ili kujadili suala lenu mapema.

Watu hao wanaweza kuwa viongozi wa dini au wanasihi na wanasaikolojia au wazee wenye busara. Chukua muda wa utulivu kufikiria juu ya tatizo lenu. Kama ulikuwa na hasira, jipe muda wa kutulia na hasira kupoa. Epuka kufanya uamuzi ukiwa na hasira kwani huwa haujengi, bali hubomoa.

Kwa kuhitimisha, ushindi katika tatizo ni kulikabili mapema. Tatizo linapojitokeza katika ndoa ni muhimu litatuliwe mapema kadri inavyowezakana. Matatizo ya ndoa kwa kawaida humalizwa na wanandoa wenyewe. Hivyo, ni muhimu wanandoa wawe na ufahamu na maarifa ya namna ya kukabili migogoro yao ya ndoa.

Mtu wa tatu anaweza kuhusishwa kwa ushauri na unasihi pale tu ambapo wanandoa watakuwa wameshindwa kutatua mgogoro wao. Wanandoa washirikiane katika kuzikabili changamoto na kuimarisha uhusiano wao.

Ndoa bila Mungu haidumu, hivyo wanandoa wamtangulize Mungu katika maisha yao, kwani baadhi ya matatizo katika ndoa hayatatuliki mpaka Mungu ahusike. Wanandoa wafahamu namna ya kuchukuliana na kusaidiana katika kasoro na upungufu yao. Kasoro ya mwenzako una nafasi ya kuirekebisha ukiamua. Kasoro za mwenzi wako ndizo zinazobeba ubora wako.

Unapoamua kumwacha mwenzi wako kwa sababu ya kasoro zake, jiulize unachotafuta ni nini? Kwani katika maisha mtu aliyekamilika hayupo. Wanandoa wanaotaka kutengana au kuachana, wasifanye haraka kutekeleza jambo hilo. Wanashauriwa kufikiri kwa uangalifu kuhusu athari zinazoweza kujitokeza katika maisha yao ya baadaye na watoto. Faraja ya watoto imo kwenye familia ya wazazi wote wawili wanaoishi pamoja na kulea kwa umoja.

• ***Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.]***

# MAISHA

FEBRUARI 21, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*




Ukurasa 10

**Kweli dada wa kazi amemuweza mwanao?**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Kuwa makini unapotafuta nyumba ya kuishi



## HARUSI

Ukurasa 12



# Jenga umbo la nyigu

Ukurasa 14

# Kweli dada wa kazi amemuweza mwanao?

**Na Moses Ismail**

BADO ni mtoto mdogo sana wa miaka mitatu au pengine anakaribia miaka minne. Kwa umri wake, hana uwezo wa kujieleza kwa maneno kwa jambo lolote analolitaka.

Lakini wewe kama mzazi, unazifahamu tabia zake. Ni mbishi wa kula, huwa hali mpaka aimbiwe nyimbo zote unazozijua na wakati mwingine mnazunguushana nyumba nzima.

Dada wa kazi aliyeondoka hivi majuzi, ndiye aliyemlea tangu alipozaliwa. Wamekuwa 'wakihaingaishana' sana juu ya tabia zake hizo za kukataa kula na wakati mwingine kulilia vitu kadhaa ambayo dada pamoja na wewe humkataza 'asivichezee' kwa kuwa ni vya hatari.

Hii ndiyo tabia yake ya asili. Naam, na ni tabia za watoto wengi wa umri wake, katika mambo kama hayo lazima mtiani mikimikiki.

Lakini tangu aondoke dada wa kazi aliyemlea tangu akiwa mchanga na kuja dada wa kazi mwingine, tabia ya mtoto wako imebadilika sana. Amekuwa akila chakula chote anachopewa na wakati mwingine kwa kujilazimisha mpaka anafikia kujitapikia na pia kila anapokatwa jambo la dada huyo anasikia na kuacha.

Kama mzazi, unashangazwa kidogo na mabadiliko haya, unafurahia hali hii ya sasa hasa unapoona mtoto wako sasa anakula vizuri na ameacha ile tabia yake ya kukataa kula. Kimoyo moyo unamsifu dada huyu mpya kwamba anajua kukaa na mtoto.

Inapotokea umeshinda nyumbani na kuamua kumlisha mtoto wako wewe mwenyewe, unagundua kuwa bado analeta 'mchezo wake' wa kukataa kula hasa kama dada hayupo karibu naye. Kwa sababu huyo, unamwambia; "ngoja nimuite dada akulishe", na ghafla mtoto anaamua kula.



Kwako kama mzazi unayemtakia mwanao afya njema na shine stahiki, jambo hili la dada 'kumdhibiti' mtoto wako katika suala la kula na kuacha mchezo mchezo linakufurahisha sana. Unashukuru sana kumpata dada wa aina hiyo.

Ni kweli, suala la mtoto kula chakula chake bila kusumbua ni jambo zuri sana. Lishe yake ni muhimu sana kwa makuzi yake. Lakini je, umetulia na kuchunguza hali anayoonyesha mtoto wako wakati akipewa chakula na dada huyu?

Ukitulia na kuangalia 'picha' nzima ya 'kulishana' chakula baina ya dada na mtoto wako, unaweza ukagundua jambo la kustusha! Ni kwamba mtoto wako hali chakula kwa furaha, bali anakula huku akiwa ametawaliwa na hofu kubwa!

Ndio ametawaliwa na hofu haswaaa! Utajiuliza, nini kinachomfanya mtoto wako awe na hofu hii? Jibu ni ukali wa dada.

Katika tafiti nyingi zilizofanywa na wataalamu wa saikolojia juu ya athari za woga na kutojiamini kwa watu wazima, hasa wale waliotoka katika familia za kipato cha kati, imebainika kuwa hali hiyo imetokana na watoto hao kunyanyaswa na madada wa nyumbani wakati wakiwa wadogo kati ya umri wa miaka 3 hadi 5.

Unyanyasaji mkubwa unaotajwa na tafiti hizo, ni ule wa ukatili wa kupigwa au kufinywa na wadada wa kazi hasa kwa watoto wenye usumbufu wa kukataa kula au utukutu wa kitoto unaosababisha kero kwa watu wanaowaangalia.

Na moja ya dalili kwamba mtoto anapitia madhira hayo, ni kuonyesha mabadiliko ya tabia kama kuamua kumaliza chakula anachopewa na dada wakazi au kufanya jambo lolote analoamrishwa pindi anapotishiwa kuwa atafanyishwa na dada wa kazi.

Inawezekana kuwa dada wa kazi aliye nyumbani kwako hana tabia hizo za ukatili na amemfanya mtoto wako kupenda kula na kuacha utundu kwa kumuonyesha mapenzi tu, lakini ni vizuri mzazi pia ukachunguza mabadiliko ya tabia za asili za utoto kwa mtoto wako ili ujue nini kimembadilisha.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

Kitenzi kifuatacho **placer** kimewekwa katika vipengele tofauti, jaribu kukinyumbua katika vipengele hivyo kwa kujaza sehemu zilizo wazi.

**Indicatif**

**présent**

| | |
|---|---|
| je | place |
| tu | places |
| il/elle | place |
| nous | plaçons |
| vous | placez |
| ils/elles | placent |

imparfait

| | |
|---|---|
| je | plaçais |
| tu | plaçais |
| il/elle | plaçait |
| nous | placions |
| vous | placiez |
| ils/elles | plaçaient |

**future simple**

| | |
|---|---|
| je | placerai |
| tu | placeras |
| il/elle | placera |
| nous | placerons |
| vous | placerez |
| ils/elles | placeront |

**passé simple**

| | |
|---|---|
| je | plaçai |
| tu | plaças |
| il/elle | plaça |
| nous | plaçâmes |
| vous | plaçâtes |
| ils/elles | placèrent |

**passé compose**

| | | |
|---|---|---|
| j' | ai | placé |
| tu | as | placé |
| il/elle | a | placé |
| nous | avons | placé |
| vous | avez | placé |
| ils/elles | ont | placé |

**plus- que – parfait**

| | | |
|---|---|---|
| j' | avais | placé |
| tu | avais | placé |
| il/elle | avait | placé |
| nous | avions | placé |
| vous | aviez | placé |
| ils/elles | avaient | placé |

**futur antérieur**

| | | |
|---|---|---|
| j' | aurai | placé |
| tu | auras | placé |
| il/elle | aura | placé |
| nous | aurons | placé |
| vous | aurez | placé |
| ils/elles | auront | place |

**passé antérieur**

| | | |
|---|---|---|
| j' | eus | placé |
| tu | eus | placé |
| il/elle | eut | placé |
| nous | eûmes | placé |
| vous | eûtes | placé |
| ils/elles | eurent | placé |


**Conditionnel**

**Present**

| | |
|---|---|
| je | placerais |
| tu | placerais |
| il/elle | placerait |
| nous | placerions |
| vous | placeriez |
| ils/elles | placeraient |

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

ANGALIA mwalimu alivyopata shida na mwanafunzi wake

**MWALIMU:** Punda ni mnyama anayefugwa nyumbani, wa mwituni pundamilia.....Je sungura anayeishi mwituni anaitwaje?"

**Mwanafunzi:** Sunguramilia.

**Mwalimu:** Kuku yuko katika jamii ya Ndege...Je samaki yuko katika jamii ya nini?"

**Mwanafunzi:** Meli

**Mwalimu:** Kocha wa Arsenal anaitwa ARSENE, wa Man-city anaitwa MANCINI.....Je wa Liverpool anaitwaje?

**Mwanafunzi:** Liver

**Mwalimu:** Kweli wewe ni kilaza mpaka unanifanya nichanganyikiwe

SWALI

Taja faida ya chakula cha muhogo

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Usiongozwe na hofu bali ujasiri kufikia malengo

KARIBU tena msomaji wangu tujadili maisha tunayopitia kila uchao. Safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo, inakupa mambo mbalimbali ya msingi ili tuvuke salama. Bado niko katika mfululizo mada kuhusu nguvu gani inayoongoza maisha yako?

Tayari nilishajadili nguvu ya hatia, chuki, hasira na wivu. Leo tuangalie hofu/woga. Kabla sijaendelea, hebu tuone tafsiri ya neno hofu kama ilivyoainishwa kwenye Oxford dictionary, "The bad feeling that you have when you are in danger" (mawazo mabaya anayokuwa nayo mtu awapo hatarini).

Kwa lugha ya kiungu, hofu ni roho inayommiliki mtu kiasi cha kumfanya akose amani muda wote na kutojiamini. Neno hofu kwa lugha ya Ki-latini, lina maana ya kuwa katika hali mbili (mawazo mawili). Mfano; mama anapokuwa mjamzito anawaza, "hivi nitajifungua salama au mimba itaharibika?" Mtu anapoanza biashara anawaza, "hivi hii biashara itanipa faida au hasara?"

Hofu ni roho kubwa inayowatesa wanadamu wengi. Ni silaha ambayo ibilisi huitumia kuwaangamiza wanadamu. Watu wengi leo wanaishi maisha ya kutojiamini kwa sababu ya hofu au woga. Wengi hawana ujasiri wakujiona kwamba wanaweza kufanikiwa.

Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi". Hofu n silaha kubwa ambayo shetani huitumia kupooza au kuua imani za watu.

Hofu humfanya shetani aongeze uwezo wa kumshambulia mwanadamu. Hii roho inapokuwa juu ya mtu inafungua mlango kwa roho nyingine kuingia na kumsababishia mateso.

Mpenzi msomaji, watu walio waoga mara nyingi wanaishi maisha ya kimaskini kwa sababu hawana uthubutu wa kuchukua hatua. Wenzao wanafanikiwa mbele yao, lakini wao wanaona ni kawaida tu, eti wamependelewa. Hapana, ni woga wako.

Ukiona mtu wa aina hiyo, ni dhahiri kuwa amefungwa na nguvu za giza zinazomfanya ashindwe kutoka. Mwingine ni roho ya ujinga inayomtesa. Mungu siku zote anataka kuona mtu anachukua hatua, ndipo naye anakungezea nguvu ya kusonga mbele. Yeye huanzia pale wewe ulipoishia kwani anakusubiri uanze ndipo akutie nguvu kuendelea. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Hofu au woga umesumbua na unaendelea kusumbua watu wengi, iwe ni wafanyakazi maofisini, wanafunzi na hata waumini. Na hii yote ni hila ya muovu shetani ili kuwatoa kwenye malengo yao. Shetani hutumia watu kusababishia wengine hofu.

Kwa mfano, wapo baadhi ya mabosi wenye viburi, hasira wanaoongoza kwa vitisho wakati wote.Hata kama wafanyakazi anaowaongoza ni wachapa kazi, badala ya kuwatia moyo yeye huwa mkali na kuwaogopesha. Ndio maana wengine wakiona kero huamua kuacha kazi. Roho za hasira, kiburi, mara nyingi zimechipua roho za hofu, woga na kutojiamini.

Msomaji wangu, pamoja na hayo, woga waweza kutokana na jambo baya lililowahi kutokea zamani. Pia malengo yasiyotekelezeka yaweza kumpa mtu hofu kwa kumzidi kimo.

Mtu anafanya biashara kisha akafilisika, kinachofuata ni woga wa kutoendelea. Binti anachumbiwa, anaachwa. Huyu ataogopa kutafuta mwenza tena kwani atahisi ni wale wale walaghai.

Woga waweza kutokana na mazingira uliyokulia. Watoto wanaweza kuwa na ubabe waliouona kwa wazazi wao. Baba na mama ni mabaunsa, wanapigana kila wakati, walevi, matusi, hawana hofu ya Mungu. Matendo mabaya ya wazazi huwatia hofu watoto, lakini wafanyeje? Tuwafundishe kuwa na ujasiri siyo woga au hofu.

Neno la Mungu linasema, 1Yohana 4:18 "Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hukamilishwa katika pendo. Pendo la Mungu likiingia ndani yako, unakuwa jasiri kama simba. Ukiona mtu ana woga, pendo la Baba mbinguni halimo ndani yake.

Kemea roho ya hofu inayokufanya uchukue uamuzi usio sahihi katika maisha yako. Jifunze kunyamazisha kila roho ya hofu inayoinuka kila unapotaka kufanya biashara yenye faida. Kwa Mungu yote yanawezekana ukimuomba kwa bidii

***Msomaji wangu, niishie hapa kwa leo. Naamini lipo jambo umejifunza kupitia ujumbe wa makala haya. Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Nitumie ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Elimu kwa umma changamoto ya upumuaji inahitajika

VIONGOZI mbalimbali wametoa tahadhari ya kuwapo kwa ugonjwa wa changamoto za upumuaji, kwa kila wananchi kuchukua hatua za kujilinda dhidi ya maambukizi kwa kuvaa barakoa, kutumia vitakasa mikono, kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni na kukaa kwa umbali unaotakiwa kwa mujibu wa taratibu za afya.

Ugonjwa huo umeshika kasi nchini kwa sasa, lakini bado kuna watu wanaendelea kuishi kwa mazoea bila kuchukua tahadhari ya kujilinda.

Katika nyumba za ibada taratibu mpya za ibada zimetolewa ikiwamo kuepuka misongamano, kunawa mikono kabla na baada, ikiwamo matumizi sahihi ya tiba asili na nyinginezo kwa haraka mtu anapohisi tofauti.

Aidha, msisitizo wa serikali ni matumizi ya tiba asili ikiwamo kupiga nyungu ambayo ni muhimu katika kuimarisha afya, na dawa nyingine zilizotolewa na taasisi mbalimbali za tiba asili.

Wananchi wangi wamesikia ushauri huo na kuanza kutumia tiba hizo ambazo zimeonyesha matumaini makubwa katika kukabiliana na changamoto za upumuaji.

Nawaza kwa sauti wakati haya yanafanyika kwenye mitaa na vyombo vya usafiri wa umma bado kasi ya kuchukua tahadhari ni ndogo na watu wanaendelea na maisha kama kawaida, jambo ambalo linapaswa kuangaliwa kwa kuwa linaweza kuongeza maambukizi.

Ni muhimu kutoa elimu kwenye mitaa na vyombo vya usafiri watu kuhakikisha wanakaa kwa umbali unaotakiwa na kuvaa barakoa, kuliko hali ilivyo katika maeneo mengi ambayo bado hawajatambua umuhimu wa tahadhari iliyotolewa.

Pia, ni muhimu kutoa elimu ya uvaaji wa barakoa kwa kuwa wapo wanaovaa na kuishusha mdomoni au kuipandisha kwenye paji la uso au kuishika mara kwa mara jambo ambalo halitakiwi kuwa hivyo, ikiwamo kuzingatia muda uliowekwa wa kuvaa barakoa za dukani.

> **"Wengine wameenda mbali zaidi na kuweka adhabu kwa wote ambao hawafuati malekezo yanayotolewa na wataalam wa afya na taratibu zilizowekwa na serikali.**

Kukiwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa umma itasaidia wengi kujikinga dhidi cha changamoto hiyo, ni vyema ukawekwa utaratibu mzuri wa kufikisha elimu kwa wananchi wengi.

Maeneo ya vijijini watu wanashiriki ibada za mazishi bila kujali hatari iliyopo kwa kukaa kwa kusongamana, kutovaa barakoa wala kunawa mikono, jambo ambalo linaonyesha zinahitajika jitihada za makusudi kuhakikisha wanaelewa umuhimu wa kuchukua tahadhari.

Dunia inateseka kwa janga la corona duniani na zipo nchi ziko chini ya uangalizi hairuhusiwi kwenda kokote zaidi ya kukaa ndani tu, na hata ukitoka upo uraratibu maalum.

Wengine wameenda mbali zaidi na kuweka adhabu kwa wote ambao hawafuati malekezo yanayotolewa na wataalam wa afya na taratibu zilizowekwa na serikali.

Hivyo, Ni muhimu sana kwa Tanzania kuchukua tahadhari zote muhimu ili kuendelea kujilinda na kuwa na afya njema.

Tayari rais John Magufuli, ameelekeza kufanyika kwa maombi ya kitaifa ya siku tatu yanayohitimishwa leo, kila mmoja kwa imani yake kumuomba Mungu kuiepusha Tanzania na changamoto za upumuaji.

Ni muhimu sana kufunga na kuomba, kila mmoja kumsihi Mungu aghairi adhabu yake dhidi ya dunia na Tanzania, kwa kuwa ndiyo wajibu wetu kuomba toba na kumuomba Mungu kwa ukamilifu ikiwamo kuishi maisha makamilifu yenye kumpendeza Mungu.

Pamoja na kusali, Mungu ametupa utashi na akili ili tuutumie kwa manufaa yetu kujikinga na majanga mbalimbali ambayo yanaweza kutuangamiza.

Ni muhimu sana kwa sasa kukawa na msisitizo wa kunawa mikono kuanzia nyumbani, sehemu za kazi, ibada na kwingine kokote ikiwamo kuvaa barakoa mtu anapokuwa kwenye mkusanyiko.

HARUSI











Kelvin Alistides Rwechungura & Carolina Samweli Mngashwa. Kanisa la Roman Catholic St.joseph lililopo Posta. Tarehe 13/02/2021



MITINDO

# Twende kiasili zaidi

MAVAZI na mapambo ya asili ya Kiafrika ni moja ya vitu ambavyo vinazidi kuwavutia baadhi ya watu hapa nchini.

Kutokana kuingiliana kwa tamaduni za nje, uvaaji wa nguo na mapambo ya kiasili yaliachwa nyuma baada ya kuonekana yamepitwa na wakati.

Hata hivyo, nguo na mapambo ya kitamaduni zimeanza kurudi tena, lakini kwa mitindo mingine ya kisasa zaidi na kuonekana kuwavutia makundi mbalimbali ya watu hasa vijana.

Moja ya mavazi na mapambo ambayo imeonekana kupendwa ni ile ya jamii ya Kimasai.

Kutokana na Wamasai kufanikiwa kwa kiasia kikubwa kulinda tamaduni zao, imekuwa rahisi kurithisha jamii zingine.

Baadhi ya vitu vinavyoonekana kusambaa na kuwa maarufu kwa watu watu mbalimbali ni pamoja na nguo, bangili na shanga.

Kutokana na hali hiyo watu wengi wamebuni njia tofauti za kuyafanya mavazi hayo na mapambo yawe ya kisasa na yaweze kutumiwa katika mazingira mbalimbali.

**MAVAZI**

Nguo zenye rangi ya bluu, nyekundu na zambarau zimekuwa pendwa na wabunifu baada ya kugundua mitindo tofauti ya magauni, mashati na suruali zenye kuegemea uasilia zaidi.

**MITANDIO**

Nguo maalum inayotumika kama mgolole yenye rangi mchanganyiko, kwa sasa inatumika kama mitandio au skafu.

**BANGILI**

Bangili za shanga moja ya mapambo ambayo wanawake wanapenda kutumia, imefikia wakati kwenye sherehe mbalimbali utaona wamevaa bangili hizo kuanzia shingoni hadi mikononi.

**VIATU**

Mitindo ya viatu unaendana na jamii husika imekuwa jambo la kawaida, viatu vyenye nakshi za shanga na vile vilivyotengenezwa kwa kutumia tairi za gari vinaendelea kupata soko kubwa.









UREMBO





# Jenga umbo la nyigu

UMBO la mwanamke ni kama dhahabu, wakati wote linatakiwa kutunzwa na kuboreshwa ili kubaki katika mwonekano wa kuvutia muda wote.

Wataalamu wa masuala ya urembo wanashauri ili mwanamke abaki katika urembo wake basi ni muhimu mwili utunzwe vizuri. Mwonekano unaovutia si ule wa wembamba kupita kiasi au unene uliopitiliza.

Kwa ujumla unapohitaji kuwa na umbo zuri, lazima uhakikishe unakuwa tumbo jembamba, mapaja yaliyoshiba kiasi, kiuno kilchokatika na shingo iliyonyooka vyema.

Hata hivyo, wengi wanajikuta wakipoteza uzuri wao baada ya kutokuwa makini kufuata utaratibu unaofaa wa kujenga mwili.

Kwa kuwezesha kuwa na umbo la kuvutia, fuatilia njia rahisi zifuatazo.

**VYAKULA**

Kama ukitaka kuondoa unene na kuwa na tumbo dogo, punguza kula vyakula vyenye wanga na nyama nyekundu, badala yake tumia mbogamboga na matunda kwa wingi. Pia punguza kula viazi mviringo, wali au mkate kwa sababu inachelewa kumeng'enywa.

**MPANGILIO WA MLO**

Kamwe hutakiwi kuwa na tabia ya kula mara kwa mara, hakikisha unakuwa na milo mitatu pekee. Usipunguze mwili kwa kujinyima chakula kwani ni hatari kwa afya yako.

**KUNYWA MAJI**

Kitu muhimu sana ni unywaji wa maji kila wakati kwani mwili unatakiwa kuwa na unyevunyevu wa kutosha ili kuzuia kuganda kwa mafuta.

Ukiweza kunywa maji ya vuguvugu kila siku asubuhi ili kusaida kuyeyusha mafuta.

**MAZOEZI**

Mazoezi ni jambo muhimu hasa katika kuondoa tumbo na kujenga kiuno, hakikisha unafanya mazoezi kila wakati kwa mpangilio mzuri.

Mazoezi ya kuendesha baskeli, kupiga pushapu au kuendesha kigari kwa mikono.

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Katlesi za samaki



KATLESI zimekuwa zikipikwa kwenye hoteli na migahawa lakini katika familia ni nadra kukuta zimepikwa kwa ajili ya mlo.

Badala ya kuendelea kula katika hoteli na maeneo mengine, leo tunawafundisha namna ya kupika katles.

**MAHITAJI**

Viazi vitano saizi ya kati, vikopo viwili vya minofu ya samaki, karoti moja, pilipili mboga nusu, kitunguu saumu nusu kijiko cha chai.

Pia andaa pilipili kiasi, chumvi kiasi, ndimu kiasi, unga wa ngano nusu kikombe, yai moja na mafuta ya kupikia kiasi.

Namna ya kuandaa

Hatua ya kwanza menya viazi uvichemshe na chumvi, vikiiva vichuje maji, viponde ponde, vilainike na vitenge pembeni.

Menya karoti iwe kama chicha, kata pilipili mboga nyembamba na fungua vikopo vya samaki.

Changanya samaki, karoti, pilipili mboga, vitunguu saumu, pilipili kali, chumvi, ndimu, na viazi ulivyoviponda na hakikisha vimechanganyika vizuri.

Tengeneza vidonge kiasi unachotaka na kata umbo unalopenda kama la yai au duwara, ukimaliza weka pembeni.

Changanya unga na maji uwe mzito, kisha weka yai na weka karai katika moto, Mimina mafuta kama ya maandazi, kisha chukua vidonge na chovya katika unga uliochanganywa yai.

Tumbukiza ndani ya mafuta yaliyopata moto vizuri na ziache mpaka zibadilike rangi ndipo uzitoe.

Katles zako zitakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa na chai, soda, maziwa au juisi.

Unaweza pia kula wakati wa asubuhi, mchana au usiku.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Kuwa makini unapotafuta nyumba ya kuishi





KUTAFUTA sehemu ya kuishi hususani kwa wanaopanga ni changamoto nyingine ambayo imekuwa ikiwasumbua watu wengi hasa katika sehemu za miji mikubwa.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi wa nyumba, Mdoe Kimbe, anasema ili upate nyumba ya kupanga kwa urahisi na ya vigezo unavyohitaji, ni lazima uviainishe na kuwasisitiza wanaokusaidia kukutafutia nyumba hiyo kuvinzingatia.

Anasema ili uishi katika nyumba yenye vigezo vyako, lazima pia uwe umejipangia bajeti ya fedha unayoimudu inayoendana na vigezo vya nyumba uitakayo.

"Ni rahisi sana kuweka vigezo kuhusu nyumba unayotamani kuishi lakini pia baadhi ya watu huwa wanaweka vigezo hivyo mwisho wa siku wanashindwa kufikia matakwa hayo kutokana na ufinyu wa bajeti zao. Ndiyo maana nasema kwamba unapoweka vigezo ni lazima pia kuwa na uhakika na bajeti yako ya fedha," anasema Kimbe.

Anashauri kwamba unapotaka kupanga nyumba, unapaswa kuangalia mahali patakapokufaa panapoendana na wewe.

"Baadhi ya watu hutamani kuishi kwenye eneo maarufu ila wanaishia kuishi maisha yale yale ambayo wangeishi kwenye eneo lisilo maarufu sana. Kwa hiyo ni muhimu kuchagua eneo ambalo linaendana na wewe.

"Kama unatafuta kujifunza aina nyingine ya maisha kutoka kwa watu tofauti uliowazoea ni vizuri kujihakikishia kama unaweza hilo ili mwisho wa siku usijione kama hufai au unatengwa," anasema.

"Kwa mfano umezoea kuishi katika eneo ambalo liko huru na una uwezo wa kuingia wakati wowote katika nyumba ya jirani, halafu inatokea unataka kubadilisha mazingira ya kwenda kuishi katika eneo ambalo utaratibu wa aina hiyo haupo, ni lazima ujiridhishe kama unaweza ili usijione mpweke.

"Kama itakuwa heri kwako kujifunza maisha mapya ya aina hiyo nalo ni sawa isipokuwa usionekane wa ajabu kwenda na utaratibu wako ambao wenzako hawakuuzoea," anasisitiza.

Kimbe anashauri kwamba ni vema pia kujiandaa kisaikolojia kwa jambo lolote linalojitokeza unapoamua kubadili mazingira ya kuishi kutoka yale uliyoyazoea na mapya.

"Huwa kuna uwezekano mkubwa wa kukutana na changamoto mbalimbali kinyume na matarajio mtu anapobadili mazingira ya kuishi, unapokutana na hali hii usikurukupe wala kuchanganyikiwa. Tulia na jifunze kutafuta ufumbuzi ulio sahihi ambao hauwezi kuleta madhara kwako na kwa familia yote," anasema Kimbe.

MPANGILIO

## Dondoo muhimu kwa ajili ya kuchagua flemu za kitanda cha mbao

**1:** Mbao za Mninga na Mkongo ni nzuri kutengeneza kitanda kutokana na mwonekano wake kuwa wa kuvutia zaidi.


**2:** Kitanda cha mbao ni bei nafuu pia kinatumika muda mrefu ukilinganisha na vingine.

**3:** Unaweza kuwekwa urembo wa aina mbalimbali na kupaka rangi kwa jinsi unavyotaka bila kuathiri michoro iliyopo kwenye mbao.

**4:** Chakua mbao ambazo hazichoki haraka ili kuondoa tatizo la kelele pale unapolalia.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

...HATA AKIKUCHEKEA, MAUMIVU BADO UNAYO....

## HABARI KIMATAIFA

# UN yataka utulivu Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

UMOJA wa Mataifa umesema una hofu kutokana na ukosefu wa usalama nchini Somalia na kuzusha mapigano kati ya vikosi vya serikali na vya upinzani.

Hata hivyo, ulitoa pia wito wa kuwapo kwa hali ya utulivu na kuzuia ghasia na pia kufanyike kwa mazungumzo ya kutatua mgogoro huo.

Katika ujumbe wake wa Twitter, ofisi ya umoja huo nchini humo, ulisema umebaini makabiliano yanayotokea mjini Mogadishu yanahitaji dharura ya viongozi wa serikali ya shirikisho na wa majimbo kukaa pamoja kufikia makubaliano ya kisiasa kuhusu utekelezwaji wa mpango wa uchaguzi.

Mgogoro huo ulizuka baada ya muhula wa Rais Mohamed Abdullahi Farmajo kumalizika siku ya Jumatatu iliyopita, huku mazungumzo ya kuandaa uchaguzi yakiwa yamevunjika.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Muungano wa Afrika, Moussa Faki Mahamat na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. General António Guterres, waliwataka pande zote mbili kuwa na moyo wa kujitolea kutatua mzozo huo.

***BBC***



Mtoto akikimbia karibu na kifaru cha jeshi katika mtaa mmoja mjini Yangon, nchini Myanmar, wakati jeshi likiendelea kudhibiti nchi hiyo baada ya kufanya mapinduzi mapema mwezi huu. **PICHA: GETTY IMAGES**

# Watoto milioni tatu hatarini DRC

**KINSHASA, DR-Congo**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia Watoto (UNICEF), limesema mamilioni ya watoto wapo hatarini katika maeneo yenye machafuko nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Katika taarifa yake, shirika hilo limesema maisha na hatma ya zaidi ya watoto milioni tatu ambao wameachwa bila ya makazi yapo hatarini.

Familia ambazo kwa sasa hazina makazi kutokana na vurugu zinaishi katika maeneo yenye msongamano wa watu, uhaba wa maji safi ya kunywa, huduma ya afya na mahitaji mengine muhimu.

Zaidi ya watu milioni 5 wamelazimishwa kuyakimbia makazi yao kutokana na vita.

Maeneo ambayo yanatajwa kuathirika zaidi ni majimbo ya Ituri, Kivu Kaskazini, Kivu Kusini na Tanganyika ambako pia inaelezwa zaidi ya watu milioni nane wana ukosefu wa chakula

***DW***

# Mshirika wa Trump adaiwa kusaidia vita Libya

**NEWYORK, Marekani**

RIPOTI ya siri ya Umoja wa Mataifa, inadai mshirika wa aliyekuwa Rais wa Marekani, Donald Trump, alimsaidia mbabe wa kivita wa Libya Khalifa Haftar kwa kumpatia silaha na mamluki wa kimataifa.

Erik Prince, ambaye ni mkandarasi binafsi wa masuala ya usalama wa Trump, alitajwa kukiuka vikwazo vya silaha nchini Libya vilivyowekwa na Umoja wa Mataifa.

Ripoti hiyo ambayo nakala yake imeonekana na magazeti ya New York Times na Washington Post, inadaiwa Prince alipeleka kikosi cha wapiganaji mamluki na silaha kwa mbabe wa kivita Khalifa Haftar, mwaka 2019 wakati akipigana kuiondoa madarakani serikali ya Libya inayoungwa mkono na umoja huo.

Operesheni hiyo ya dola milioni 80, ilijumuisha mipango ya kuunda kikosi kitakachowafuatilia na kuwaua makamanda wa serikali wanaompinga Haftar, pamoja na wadau wengine ambao walikuwa raia wa mataifa ya Umoja wa Ulaya, limesema gazeti la New York Times.

Kulingana na jopo la wataalamu, Prince akiwa mjini Cairo mwaka 2019 alipendekeza operesheni ya kijeshi ya kumsaidia Haftar kupambana na serikali ya Libya inayotambuliwa kimataifa.

Ripoti hiyo ilisema kama sehemu ya kile kilichoitwa "Operesheni Opus", Prince alipendekeza kumsaidia Haftar kwa ndege na meli za kivita pamoja na kushirikiana nae katika kuandaa mpango wa kuwateka nyara mahasimu wake wa ngazi za juu.

Inazidi kueleza kufuatia makubaliano hayo, Prince alituma ndege za kivita nchini Libya na kuikiuka marufuku ya Umoja wa Mataifa ya kuingiza silaha nchini humo.

Prince, ni mwanajeshi wa zamani wa kikosi cha majini cha Marekani na ndugu wa aliyekuwa waziri wa elimu Betsy DeVos, amekuwa mshirika wa karibu wa Trump katika miaka ya hivi karibuni.

**DW**

# Wafanyakazi wa Rais Sudan waambukizwa Covid-19

**JUBA. Sudan Kusini**

WAFANYAKAZI 27 wa ofisi ya rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir, wamekutwa na maambukizi ya virusi vya Corona.

Walioathirika na ugonjwa huo ni wafanyakazi wa ngazi ya chini na walinzi wa kiongozi huyo.

Hata hivyo, Rais Kiir hajapatikana na virusi hivyo, kulingana na msemaji wake Ateny Wek Ateny.

"Ni kweli, zaidi ya wafanyakazi 20 wamepatikana na virusi, hasa wale wa kitengo cha ulinzi na wafanyakazi wa ngazi ya chini katika ofisi ya rais," alisema

Aliongeza "Mimi ni mmoja wa maofisa wawili wa ngazi ya juu walipatikana na corona, mimi na mchambuzi wa sera tunafikia ya jumla watu 27,"

Alisema kuwa wafanyakazi wote walioko Ikulu ya kiongozi huyo katika mji mkuu Juba watapima tena kwa awamu ya pili kama tahadhari.

Mawaziri wawili na mshauri wa rais pia walipimwa mara ya pili.

***BBC***

MAKALA

# TUNA LA KUJIFUNZA KUTOKA KWA MAALIM SEIF KATIKA SIASA ZETU?



Na Magabilo Masambu

AWALI ya yote, nitumie nafasi hii kuwapa pole Wazanzibari na Watanzania wote juu ya misiba mikubwa iliyotufika katika juma hili. Kuwapoteza viongozi wakubwa kabisa katika taifa. Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharifu pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, poleni sana Watanzania wenzangu.

Kila mara inapotokea misiba inatukumbusha wale tunaobaki kuhusu maisha na harakati za wapendwa wetu waliotutangulia. Ni muhimu sana kujitafakari kwa kina ikiwa ni sehemu ya kujifunza kurekebisha au kufuata nyayo zao kwaaajili ya mustakabali wa maisha yetu.

Leo tutazame mambo machache ambayo nafikiri tunaweza kujifunza kutokana na maisha, harakati za wanasiasa hawa zaidi nikijikita kwa ndugu Maalim kama mwanasiasa nguli na mashuhuri.

Nasema ndiyo tuna la kujifunza kutokana na harakati na aina ya siasa za Maalim, kama taifa na wananchi wa Tanzania. Si tu kujifunza bali kuchukua hatua ya kimatendo ili kuendeleza mazuri aliyoyafanya mzee wetu katika siasa za Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Moja, juu ya usitahimilivu na uvumilivu. Maalim ni mwanasiasa aliyekuwa wa aina yake. Historia inaonyesha ameanza harakati za siasa miaka mingi iliyopita tangu tu alipohitimu masomo yake katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam mnamo mwaka 1975 katika sayansi ya siasa.

Baada ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 na uchaguzi wa kwanza wa mwaka 1995, Maalim amekuwa na harakati katika nafasi mbalimbali zaidi akiwa mgombea wa ngazi ya urais mpaka mauti unamkuta hajawahi kukata tamaa.

Hili ni liwe funzo kubwa kwa vijana wanao kata tamaa mapema wanapozikosa nafasi wanazozitafuta na kupelekea ama kuacha siasa ama kuhamahama vyama vya siasa kutafuta urahisi wa kuyapata madaraka.

Pili, alivyoweza kujitengenezea wafuasi wengi wa hiari. Maalim ilifika mahali akawa kama taasisi kamili na alivuka kuvuka mipaka ya kuitwa mwanasiasa tu, bali alikuwa kama taasisi iliyosimama peke yake. Kwenye siasa mara nyingi wanasaisa huwa na wafuasi wenye nia mbalimbali, wengine wanakuwa wafuasi wako kwa sababu wanategemea madaraka kutoka kwako.

Wengine wanaweza kuwa wafuasi kwa sababu zinatumika njia za kuwalazimisha wawe, lakini kwa Maalim ilikuwa tofauti ndiyo maana alipotangaza kukihama chama chake alichokiasisi (CUF) akaenda ACT WAZALENDO karibu Zanzibar nzima ilibadilika na kuwa zambarau. Wanasiasa wakongwe na vijana wanajambo la kujifunza hapa namna bora ya kuwa na wafuasi wa aina ya wafuasi wa Maalim.

Tatu, ni aina ya siasa alizokuwa akiziamini. Maalim alikuwa muumini wa kuamini siasa za maridhiano, yaani siasa za pamoja. Leo ameondoka lakini amewaachia Wazanzibari umoja. Nichukue nafasi kumpongeza pia Daktari Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar, kwa uungwana wake wa kuona kwamba kama Wazanzibari wanahitaji kuwa pamoja wakaridhiana na Maalimu kuwa na serikali ya umoja.

Pengine jambo hili limechukuliwa kwa namna tofauti na watu tofauti lakini ukweli utabaki palepale kwamba ni muhimu Wazanzibari kuweka tofauti zao za kisiasa pembeni na kuijenga Zanzibar, katika hili Maalim atakumbukwa katika historia za siasa za Zanzibar.

Nne, tuna la kujifunza juu ya kutengeneza taasisi imara kuliko kutengeneza watu imara kwenye taasisi. Sababu kubwa hapa ni kwamba mwanadamu anazaliwa na ataondoka siku moja kama ambavyo maandiko kutoka katika vitabu mbalimbali vya dini yanavyosema.

Tukijikita katika kutengeneza taasisi imara zenye Sheria imara yeyote anaweza kuwa kiongozi na mambo yakaenda vizuri kabisa bila shida. Simaanishi kwamba kuondoka kwa Maalim kutasababisha chama kuyumba lakini inaweza kuwachukua muda kidogo kuwa na mtu kama Maalim lakini kama taasisi ikiwa imara inaweza kuwa imetengeneza akina Maalim wengi zaidi.

Bahati mbaya tu Afrika tunadhani kuwa na watu imara kwenye nafasi za uongozi ni bora kuliko kuwa na taasisi imara ambazo zinatakiwa kuwasimamia watu hao. Tuweke mifumo imara tuwache kuwategemea binadamu ambao siku moja hawatakuwapo na inapotokea hivyo basi inakuwa kama taasisi hizo zinaanza upya katika kuweka utaratibu wa kujiongoza.

Mwisho, tuyaamini mazungumzo ya mezani zaidi katika kutatua changamoto zetu kama taifa kuliko njia nyinginezo ambazo zinaweza kuleta maumivu badala ya umoja miongozi mwetu. Maalim aliamini sana kwenye mazungumzo lakini pia viongozi mashuhuri zaidi duniani hutumia njia hii kuleta maelewano pasipo maelewano.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***ARUSHA-TANZANIA***

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Riwaya ya 'Allan Quatermain' iliyowapa ujasiri vijana



Na Adam Fungamwango

SIKU hizi vijana wengi si wasomi wazuri sana vitabu kama ilivyo zamani. Labda huwa wanavisoma kwenye simu za mkononi ambazo siku hizi zina kila kitu.

Lakini kwa uchunguzi wangu mdogo ni kwamba vijana wengi wa kisasa ni wavivu kusoma, badala yake wanapenda sana kuangalia. Yaani wanapenda zaidi kuangalia filamu kuliko kusoma.

Kuna utofauti kidogo kati ya kuangalia na kusoma. Filamu huonyesha moja kwa moja mazingira yaliyopo na kwa sababu mtu anaangalia hafikirishi zaidi ubongo. Na wanaoangalia wote wanakuwa wanaone kitu kile kile. Lakini wanaosoma riwaya au hadithi, kila mtu anatengeneza taswira kivyake kichwani.

Miaka ya nyuma kulikuwa na vitabu vingi ambavyo kijana yeyote ili akamilike ni lazima avisome. Kuna vya watoto, halafu vya vijana. Kijana anapofika umri kuanzia miaka 15, anaanza kuvisoma. Viko vingi, lakini leo tuataanza na kitabu kimoja maarufu mno cha 'Allan Quaterman'.

Sidhani kama vijana wa enzi hizo ambazo kwa sasa ni watu wazima hawajavisoma. Nafikiri asilimia 90 ya vijana wengi wa Kitanzania miaka hiyo wamekisoma. Hata asilimia ndogo iliyobaki ambao hawajakisoma, watakuwa wamekipitia angalau kurasa tatu nne, au nusu. Hata hata vyote hivyo mtu hajapitia, atakuwa anasikia habari au simulizi za kitabu hicho.

Nadhani ndicho kitabu maarufu zaidi enzi hizo. Kilitungwa na mzungu mmoja anaitwa Sir. H Rider Haggard kwa lugha ya Kiingereza lakini kilitafsiriwa Kiswahili na kutoka Januari Mosi, 1955 na kupendwa sana hapa nchini, wakati huo ikiitwa Tanganyika na hata baada ya Uhuru, ikaitwa Tanzania.

Mtunzi alikitunga kitabu hiki kutolewa rasmi mwaka 1887 kwa lugha ya Kiingereza.

Ni simulizi au kisa cha mwindaji wa tembo Bwana Allan Quatermain au kwa jina lingine Makumazan.

Huyo jamaa alikuwa na wasaidizi wake Msolopagazi, ambaye alikuwa na shoka lake kali alilolibatiza jina la Inkoskazi. Pia kulikuwa na wahusika wengine kama Bwana Henry Curtis na rafiki yake Sir Good. Kwenye riwaya hiyo, anapatikana bibi mmoja mchawi anaitwa Gagula.

Vijana wa kisasa, wakimisi mtu machawi, wanamwita 'kikagula', lakini sidhani wengi wanajua jina hilo limetokea wapi. Ni kwenye kitabu hicho ndipo alipopatikana kibibi hicho Gagula ambaye ndiye jina lake, lakini akiwa na sifa ya uchawi, ndiyo ukazuka msamiati kwa vijana wa sasa.

Ni miongoni mwa riwaya zinazoonyesha au kusimulia ujasiri na ushujaa wa hali ya juu sana.

Hii ni moja riwaya chache duniani yenye maneno yenye hisia kali ambayo yanaingia ndani ya moyo na ubongo wa mtu na kumfanya abadilike. Hapo ndipo baadhi ya watoto walianza kubadilika na kuwa watukutu, wengine wagomvi, wababe, watemi, ujasiri na mashujaa pia.

Kitabu hiki kiliwabadilisha baadhi ya vijana kutumia vibaya maneno yaliyomo kwenye riwaya hiyo na kikapigwa marufuku kwenye miaka ya 1970. Kutokana na hali hiyo kikaacha kuchapishwa na watu wakawa wanaazimana tu vilivyopo. Hata hivyo kwa sasa vipo na vinauzwa kwenye maduka mbalimbali ya vitabu, ingawa si vijana wengi wanaojua hilo.

Ni vitabu vizuri sana kuvisoma kwa vijana wa sasa kama wanataka kuwa majasiri, na kuutumia vizuri kwa manufaa yao, familia zao, sehemu wanaozoishi na nchi kwa ujumla.

Kwa wale vijana wa zamani, walikuwa wazikariri baadhi ya maneno yaliyomo kwenye riwaya hiyo. Hutoonekana mjanja kama kijana hautokariri baadhi ya mistrari iliyomo kwenye riwaya hiyo ya kale.

Vijana walikutana wakakati mwingine na kushindana, kila mmoja akitoa mistari yake aliyoikariri kwenye kitabu hiyo, hivyo kuwa burudani tosha kwa wale wanaowasikiliza. Hadi leo hii ndiyo riwaya ambayo vijana wa wakati huo ambao kwa sasa wengi wao ni watu wazima, wazee na vikongwe na huenda wakawa wana matatizo ya kusahau, lakini hawawezi kusahau baadhi ya mistari au maneno yaliyomo kwenye kitabu hicho.

Tu tayari! Tunainoa midomo yetu kama tai, mikuki yetu inang'aa katika miali ya Jua; twaitikisa mikuki yetu tuna njaa ya kupigana. Nani anayekuja kumwamkia Inkosikazi? Nani anataka kumbusu yeye ambaye matunda ya kubusu kwake ni kufa?

Mimi Gotagota, mimi mwuaji, mimi mwenye mbio, mimi Umslopagaas mwenye shoka, wa kabila la Kizulu, mkuu wa kikosi cha Nkomabakosi: mimi Umslopogaas, mwana wa ulimi wa Mfalme, mwana wa Makedama, mtoto wa Mosilikaatze, mimi, wa damu ya Mfalme Chaka, mimi, mshindi wa wasio shindika, mimi nawaita kama kulungu aitwavyo, nawakaribisha, nawangojea. Aha! Ni wewe, ni wewe! Hii ni moja ya nukuu kweye kitabu hicho.

"Nakufa, nakufa lakini vilikuwa vita vya Kifalme. Wako wapi wale walioipanda ngazi kuu? Siwaoni. Wewe upo Makumazan, au umekwisha nitangulia katika mahali pa giza ninakokwenda mimi? Damu inanipofusha - mahali panazungukazunguka - nasikia ngurumo ya maji: ninaitwa!"

Hii ni baadhi ya misemo maarufu ya kishujaa na kijasiri inayonukuliwa sana na wasomaji ndani ya riwaya hiyo.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risassi zilimfanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmåoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya Toyata IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-10

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

“NEEMA. Kutana na Ester hapa.” Jerry alianza utambulisho.

“Huyu ni rafiki yangu, alikuwa mpenzi wangu wakati toko chuo lakini alihama na hatukuonana tena. Milima haikutani binadamu wanakutana. Tumebahatika kuonana wiki mbili zilizopita maeneo ya Mtoni. Inawezekana kabisa saa hizi angekuwa mke wangu. Lakini ndiyo basi tena. Ameolewa.”

Alipoongea neno la mwisho, alimtazama Ester ambaye aliona anaangalia chini.

“Ester. Huyu ni rafiki yangu pia. Anaitwa Neema. Huyu nilikutana naye Makumbusho, nikampenda na nikawa nimeweka dhamira nimuoe. Lakini sikujua kumbe amesholewa na ana mtoto mmoja kama wewe.” Jerry aliendelea na utambulisho.

“Pamoja na kuwa ameolewa, lakini bado ameendelea kuwa rafiki yangu wa kawaida tu, na tunasaidiana kwenye shida na raha. Kwa hiyo hapa nina wanawake wawili ambao kwangu tena si riziki yangu.” Alisema na kuwatazama kwa zamu. Walionekana kuwa hamu ya kutaka kujua kinachoendelea.

Kila mmoja alitaraji kuna cha ziada. Hakudhani kama Jerry aliwaita kwa ajili ya kuwafagamisha kuwa mmoja alikuwa mpenzi wake na mwingine alitaka kumuoa, lakini kumbe ni mke mtu.

“Nilichowaita hapa wote wawili ni kwamba kila mmoja alinieleza matatizo yake kwa nyakati tofauti.

Na ninyi hapa kila mmoja akataka nimsaidie. Na kweli nimeamua niwasaidie. Kwa uchunguzi nilioufanya nimegundua kuwa kesi yenu inafanana. Neema na Ester matatizo yenu ni hayo hayo.


Kwa maana hiyo, nyinyi wenyewe mnatakiwa muongee, myajenge na myamalize.

Kwa mara ya kwanza Neema na Ester walitazamana usoni. Kila mmoja akiwa anataka kupata picha ya mwenzake na kwa nini matatizo yao yanafanana. Kila mmoja ana shida yake ambayo anaamini ni kubwa mno na ngumu kutatulika kwa hali ya kawaida.

Leo Jerry anasema tatizo lao ni moja tu.

“Mimi nitakuwa nawapa ushauri nini cha kufanya na kuwaweka sawa, lakini nyinyi hapa wanawake wawili mkizungumza vizuri, kila mmoja tatizo lake litakuwa limetatulika au kumalizika kabisa.”

***********************




**“Ester, hili niachie mimi. Huyu mtoto atafika kwa wazazi wake. Atarudi vizuri tu na si rafiki wa mjomba wake, mjomba wake, mkewe wala wewe mtakaopata msukosuko wowote, achilia mbali kukamatwa.”**

Akiwa ametoka kidogo kwenda kuwanunulia chakula wageni wake, Jerry aliikumbuka siku ambayo aliitwa na Ester kwenda nyumbani kwake Ubungo.

Alichoshangaa ni kwamba sehemu ambayo alipelekwa aliwahi kufika siku moja. Ni siku ambayo alikuwa anamfukuza yule mtu ambaye alimteka mtoto wa Neema.

Geti lilifunguliwa. Mlinzi alikuwa yule yule. Alipelekwa ndani ya kutambulishwa. Baada ya chakula Ester alianza kueleza kilichomsibu.

“Na huyu hapa unayemuona ni mtoto ambaye alitekwa na rafiki wa mjomba wangu. Ulikuwa ushauri wake, wala si mimi au mjomba.” Ester alimalizia baada ya mjadala wa muda mrefu.

Wakati wote huo Jerry hakusema kitu chochote ambacho anakifahamu kuhusu mtoto huyo.

Wala hakusema kuwa anamfahamu.

“Sawa, mimi nimekuelewa. Kwa hilo mimi nitakusaidia, lakini kwa sharti moja tu.” Jerry alinguruma.

“Sharti gani?”

“Mtoto arudishwe kwao.”

“Sawa atarudishwaje wakati alitekwa? Tukamletekeze sehemu au, maana haya yeye aliyemteka anaogopa kukamatwa. Huwezi kuwarudishia wenyewe, wala polisi.”

“Ester, hili niachie mimi. Huyu mtoto atafika kwa wazazi wake. Atarudi vizuri tu na si rafiki wa mjomba wake, mjomba wake, mkewe wala wewe mtakaopata msukosuko wowote, achilia mbali kukamatwa.”

Maneno hayo yalimshangaza Ester. Pia akamshangaa aliyekuwa akiongea hayo maneno. Alionyesha kama ni mtu mwenye mamlaka.

Ni kwamba hali ile ilimuumuza Ester na kuomba ushauri. Alidhani labda kungekuwa na ugumu mno au kutumia muda mrefu, badala yake Jerry alikuwa akijibu kwa urahisi zaidi kama vile mtu ambaye alikuwa amepangilia maneno hayo kabla.

alichokuwa hakijui Ester ni kwamba Jery alimfahamu mtoto huyo kuwa anaitwa Diana. Alitekwa na mtu mmoja aliyekuwa akiendesha Toyota IST maeneo ya Keko Bora mwezi mmoja uliopita.

Na yeye alimfuatilia mtekaji kwa kutumia bodaboda ya kukodi hadi pale Ubungo Maziwa, gari hilo lilipomezwa na geti lililofunguliwa ikaingia. Ndiyo maana alikuwa alikuwa anaelewa vitu vingi ambavyo vilimshangaza Ester ambaye hakutaka mshirika yoyote kwenye mjadala huo.

“Nikimaliza mjadala na wewe ndiyo nitaongea na mjomba, yeye hawezi kupinga.”

“Sawa, lakini kwanza kabla ya yote, mtoto yupo kwenye hali gani?”

“Yaani huwezi kuamini, yuko salama salimini. Ni kweli alipofika hapa alikuwa anaumwa.

Tulimwita dokta wa watoto alimtibia, akapona kabisa. Mwanzoni alitusumbua kwa kulia, lakini kwa sasa ameshazoea. Kwa sasa kama nyumbani kwao, anacheza tu na mwenzake Tina.”

“Sawa Ester, kama afya yake iko vizuri, basi hilo niachie mimi. Huyu mtoto atafika tu kwa wazazi wake bila wasiwasi.”

“Unamfikishaje?”

“Kwani alitekwa wapi?”

“Nimeambiwa Keko Bora.”

“Basi nitaanzia hapo.”

“Si itakuwa hatari kwako, utaonekana wewe ndiyo umefanya hivyo?”

“Kumbuka kuwa umeniita ili nikupe ushauri na ikiwezekana nikusaidie, sawa?”

“Sawa.”

“Sasa tulia, we angalia huu mchezo mimi nitauchezaje. Nitaucheza kwa amani na utulivu. Hakuna atakayekamatwa si mimi, wala ninyi.”

Hayo yalikuwa majadiliano yaliyofanyika siku hiyo. Ndipo Jerry alipojua kuwa Diana yupo hai na mzima wa afya na ndipo mpango wa kumrudisha kwa wazazi wake ulipofanyika.

Wakati kwa Ester likionekana kuwa ni gumu, lakini kwa Jerry lilikuwa rahisi tu, kwani atakayerudishiwa ni mama yake Neema ambaye anammudu.

**************************

“Aliyetaka chips kuku na maji ya Kilimanjaro ni nani?” Aliuliza kama vile alikuwa hajui aliyemwagiza.

Ester na Neema waliangua vicheko.

“Si umpe yeyote yule.” Neema alidakia. Jerry alijua oda ile haikuwa ya Neema bali Ester, ila utani ulikuwa jadi yake.

“Haya na wewe chukua oda yako ya chips mayai na soda.” Hii sasa alimkabidhi Neema. Alianza kuwatania kwanza kwa dakika tano nzima ili wafurahie chakula.

“Enhee, mmefikia wapi?” Aliuliza.

“Jerry, ni kwamba nimeongea na mwanamke mwenzangu. Tumeongea mengi sana. Kusema kweli ni mtu mzuri na mwelewa sana. Amenipa ushirikiano mkubwa na kasema atazidi kunipa ushirikiano huko mbele ya safari.” Alisema Ester alionekana mchangamfu zaidi kuliko mwanzo alipokuja.

“Eti Neema ni ya ukweli hayo?”

“Ni kweli, ameniambia mtoto yupo kwao. Tumeongea mengi. Tumeongea kila kitu. Mimi nimeshukuru kwa sababu amenihakikisha kuwa mtoto ni mzima, tena wa afya na alikuwa alimlea kama mama.” Neema alijibu.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# KIM KARDASHIAN AOMBA TALAKA KINGUVU

HATIMAYE mwanamitindo na mshiriki wa vipindi vya televisheni wa nchini Marekani, Kim Kardashian, amethibitisha kuwa ametoa ombi la kudai talaka kutoka kwa mume wake Kanye West.

Ndoa ya kati ya Kim na rapa maarufu, Kanye imedumu kwa muda wa miaka sita na miezi kadhaa na imekuwa 'kapo' inayofuatiliwa na watu wengi duniani.

Kupitia wakili wake, amewasilisha mchakato wa talaka lakini bado imekuwa siri chanzo cha kuchukua hatua hiyo.

Taharuki ilitanda juu ya mahusiano yao kwa miezi kadhaa ikielezwa kuwa wawili hao ambao wana watoto wanne wametengana na wapo katika utaratibu wa kuachana.

## Maskini Angella augua ugonjwa usiojulikana

MWANAMUZIKI wa kike anayekuja kwa kasi, Angella, amesema ugonjwa wa miguu unaomsumbua ulianza kujitokeza wakati akiwa darasa la saba.

Anjella ambaye anasaidiwa kwa karibu na msanii maarufu wa Bongo Fleva, Harmonize, ameeleza amepambana sana na matibabu ya ugonjwa huo, mpaka alikata tamaa kama ipo siku atarudi katika hali yake.

Hata hivyo, amemshukuru Harmonize kwa kumuahidi kumpeleka nchini India kwa ajili ya matibabu.

"Tatizo la miguu lilianza nikiwa darasa saba sasa imepita miaka nane, nililala na nilivyoamka mguu ukawa unauma, tukakaa kama wiki ukaanza kutoa uvimbe, tukaenda Hospitali ya kwanza Ugonjwa hakuonekana ya pili wakasema ni tende, ya tatu wakasema mirija inayopitisha uchafu imeziba". Amsema Anjella



## Abbah atambulisha 'Blessings' na Jux

PRODYUZA maarufu wa muziki nchini, Abbah, ameaichia ngoma mpya 'Blessings' akimshirikisha mwanamuziki Juma Jux.

Wimbo huo unapatikana kwenye album yake mpya ya 'The Evolution' anayotarajia kuizindua wiki inayokuja.

Abbah anatarajia kufanya uzinduzi wa aina yake February 27, mwaka huu jijini Mwanza, akiwa na wasanii wengine kama Darassa na Marioo.



# Ancelotti amtetea Rodriguez Everton

**LIVERPOOL,** England

CARLO Ancelotti amekanusha uvumi kwamba, James Rodriguez anaweza kuondoka Everton, akisisitiza mchezaji huyo ana "furaha" klabuni hapo.

Ripoti zilibainisha kwamba, James, ambaye alijiunga na Everton kutoka Real Madrid Septemba mwaka jana, hana furaha na anafikiria kwenda Atletico Madrid.

Lakini Ancelotti amekanusha madai hayo kabla ya mchezo wao wa jana Jumamosi dhidi ya Liverpool.

"Yupo poa, hana tatizo. Nazungumza naye kila siku, ana furaha hapa, anajiamini na ana hamasa kubwa," alisema kocha huyo wa Everton akiwaambia waandishi wa habari.

"Alikuwa na tatizo kidogo kwenye mechi zake zilizopita kwenye kigimbi cha mguu. Lakini sasa yupo kwenye hali nzuri. Anajisikia vizuri hapa, kwa sababu kila mmoja anamjali yeye na hiyo ndio sababu.

"Sijui kama analalamika kuhusu hali ya hewa, lakini tunajua kwamba hali ya hewa ya hapa si bora kabisa, lakini kuna vitu vingi vizuri eneo hili."

James amefunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho tatu kwenye mechi 17 za Ligi Kuu msimu huu.






# BARCELONA YAFUNGUKA KUMGOMEA FATI UTD

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona ilikataa ofa ya euro milioni 150 kutoka Manchester United kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji wake kinda, Ansu Fati.

Fati alikuwa mmoja wa wachezaji waliolengwa na Man United kipindi cha majira ya joto kilichopita, baada ya kung'ara sana pale Nou Camp.

Lakini ofa ya Man United ya euro milioni 150 ilikataliwa na Barcelona ili kumuachia Fati, kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo.

Klabu pia ilichagua kukataa ofa kwa Pedri na Francisco Trincao msimu huo wa joto, Bayern Munich pia ilitaka kuwasajili wachezaji hao katika dirisha la majira hayo.

Fati kwa sasa bado anajiuguza baada ya kuumia mwanzoni mwa msimu huu na anatarajiwa kurudi dimbani Aprili mwaka huu.

# Mourinho: Nataka Kane acheze kila mechi

**LONDON,** England

JOSE Mourinho anamtaka Harry Kane kucheza "kila dakika ya kila mechi" lakini amesema kwamba, kinara huyo wa mabao Tottenham Alhamisi alitakiwa kupumzika kwa ajili ya kujitazamia hali yake kiafya.

Kane alipata tatizo la kifundo cha mguu kwenye mchezo wa kichapo kutoka kwa Liverpool Januari 28 na anaonekana anaweza kukosa wiki kadhaa tangu aliporejea dimbani kwenye mchezo dhidi ya West Brom Februari 7, mwaka huu.

Ilikuwa ni hatua ambayo iliwapa Spurs ushindi wa mabao 2-0 na ulikuwa ushindi pekee ambao walipata katika michezo mitano iliyopita.

Baada ya kupoteza kwa Everton katika michuano ya FA na kichapo kutoka kwa Manchester City wiki iliyopita, Kane hakuweza kusafiri mpaka Budapest kwa mchezo wa kwanza wa Ligi ya Europa dhidi ya Wolfsberger, Alhamisi

Tottenham walifanya kazi yao bila nyota wao Kane, lakini Son Heung-min, Gareth Bale, Lucas Moura na Carlos Vinicius kila mmoja alifunga bao moja katika ushindi wa 4-1 wakiwa na faida ya mabao manne ugenini.

"Anajua kwamba namtaka kucheza kila dakika ya kila mechi kwa hiyo si suala la kuchagua," alisema Mourinho akiwaambia waandishi alipoulizwa kuhusu Kane.

"Yeye mwenye anafahamu kwamba, namhitaji, lakini majeraha yake ya mara kwa mara ndio yanayofanya nishindwe kumtumia.

"Ni mchezaji muhimu sana kwa Tottenham, hivyo uwapo wake kikosini ni jambo muhimu sana kwetu sisi."

Kane amekuwa mfungaji bora msimu huu akiwa na Son akifunga mabao 13 wakati pia nahodha huyo wa England ametoa pasi za mwisho 11.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN CITY SASA YAMKANA MESSI

## ●●● Klabu hiyo haijaweka ofa yoyote mezani na hakuna mazungumzo yoyote ambayo...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City imeamua kujiweka mbali na kuhusishwa kwao na uhamisho wa mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi.

**Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina mkataba wake wa sasa unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja.**

Huku Barcelona ikionekana inaweza kuondolewa mapema kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kumezidisha uvumi wa nyota huyo kutaka kuondoka pale kwenye dimba la Nou Camp.

Wakati uchaguzi wa rais wa klabu hiyo ukitarajiwa kufanyika hivi karibuni, wagombea wote wamejigamba kwamba, wanaweza kumbakiza nyota huyo mwenye umri wa miaka 33.

Messi ameshinda mara sita Ballon D'Or katika maisha yake ya soka na kuchukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora kabisa duniani kwa sasa.

City kwa muda mrefu imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumchukua nyota huyo, hasa kutokana na kocha wao Pep Guardiola kuwa mtu wa karibu na Messi, huku pia Paris St-Germain ikitajwa kumuwania.

Na sasa imeripotiwa kwamba, City haijaweka ofa yoyote mezani kwa ajili ya Messi na BBC Sport imethibitisha kutoka chanzo kimoja ndani ya klabu hiyo kuwa hakuna mazungumzo yoyote yaliyofanyika.

Messi alionekana kama angejiunga na City baada ya kuwasilisha maombi ya kutaka kuondoka Agosti, mwaka jana kabla ya kuamua kubaki kwa nguvu kubwa ya rais wa wakati huo, Josep Maria Bartomeu ambaye alijiuzulu Oktoba mwaka jana.

## ZISIKUPITE

### MOURINHO HALI TETE SPURS

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, anataka kusubiri hadi mwishoni mwa msimu ili kutathimia majaliwa ya kocha wake mkuu, Jose Mourinho. ***(ESPN)***

### AGUERO HAJUI HATIMA YAKE

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, amebainisha kwamba, hajui kama msimu huu utakuwa wa mwisho kwake kucheza pale Manchester City. ***(Times)***

### MESSI HAJAAMUA BADO

NYOTA wa Barcelona na Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, bado hajaamua wapi atacheza msimu ujao na wawakilishi wake hawajafanya mazungumzo na klabu yoyote. ***(ESPN)***

### SOLSKAJAER KUTETA NA CAVANI

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer, amethibitisha kwamba atafanya mazungumzo na sttraika wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, kuhusu kuongeza mkataba wake pale Manchester United. ***(Sky Sports)***

### TUCHEL KUMBAKIZA PULISIC

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amemtaka winga wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 22, kubaki hapo Stamford Bridge, lakini amesema hakuna maamuzi yoyote yaliyofikiwa hadi sasa. ***(London Evening Standard)***

### KEPA ATOA LA MOYONI

GOLIKIPA wa Chelsea na Hispania, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 26, amedai kamwe hakutaka kuondoka klabuni hapo na hakuwa na hofu kuhusu kugombea namba. ***(Star)***

### SANCHO KUUZWA

KLABU ya Borussia Dortmund ingependa kumuuza mshambuliaji wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20 na kumbakiza straika wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye miaka 20. ***(Bild)***

### SMITH AMKATAA KONSA

KOCHA wa Aston Villa, Dean Smith, amekanusha uvumi wa kuhusishwa na mlinzi wa England, Ezri Konsa mwenye umri wa miaka 23, huku Liverpool na Tottenham nazo zikimuwania. ***(Birmingham Mail)***

### GIANLUIGI KULIPWA ZAIDI

GOLIKIPA wa AC Milan na Italia, Gianluigi Donnarumma mwenye umri wa miaka 21, anataka kuwa kipa anayelipwa zaidi duniani. Mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu na PSG na Chelsea zinamuwania. ***(90min)***

### MILIK, MARSEILLE HADHARANI

STRAIKA wa Poland, Arkadiusz Milik mwenye umri wa miaka 26, kwenye mkataba wake na Marseille ana kipengele cha euro milioni 12 kama klabu ikitaka kumnunua. ***(Calciomercato)***

## HABARI MICHEZO

### Zaydi nje wiki sita Domayo akirejea

**Na Saada Akida**

KIUNGO Mshambuliaji wa Azam FC, Yahaya Zaydi, atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa wiki Sita baada ya kuumia bega kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbeya City uliopigwa Alhamisi iliyopita katika Uwanja wa Azam Complex.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria, alisema Zaydi hatakuwapo kwenye mechi ijayo kwa sababu ya kupata majeraha ya bega na kutakiwa kukaa nje ya uwanja kwa kipindi cha wiki Sita kwa ajili ya matibabu.

Alisema ataanza kuikosa mechi ya leo dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja Azam Complex.

"Lakini pia kuna habari njema kwa kiungo wetu, Frank Domayo, amerejea na kuanzia Jumatatu ataanza mazoezi mepesi, bado tukiendelea kuwakosa Salum Abubakary (Sure Boy) na Obren Chirwa ambao wanendelea na matibabu," alisema Zakaria.

Alisema pia wamepokea barua kutoka Zimbabwe kuhusu mshambuliaji wao, Price Dube, kutakiwa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya nchini hiyo kwa ajili ya mechi mbili za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) dhidi ya Botswana na Zambia.

### Simbu ajiweka fiti kwa Kili Marathon

**Na Shufaa Lyimo**

MWANARIADHA Alphonce Simbu, amesema anaendelea na mazoezi makali kujiandaa na mbio za Kilimanjaro Marathon zinazotarajiwa kufanyika Februari 28, mwaka huu, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Mashindano hayo yatashirikisha wanariadha mbalimbali kutoka nje ya nchi hususan ni katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

Akizungumza na gazeti hili wiki hii akiwa mkoani Arusha, mwanariadha huyo alisema anaendelea na mazoezi ya kukimbia ili kujiweka tayari kwa mbio hizo ambazo amepania kuibuka na medali.

"Ninaendelea na mazoezi nje ya Jiji la Arusha kwa lengo la kwenda kufanya vizuri katika mashindano hayo mwaka huu," alisema Simbu.

Aidha, Simbu alisema anatarajia kukutana na ushindani mkubwa hasa kutoka kwa wanariadha kutoka nje ya nchi.

Alisema mazoezi yake anayafanya akiwa chini ya makocha wake wawili, Antony Muingereza pamoja na Philipo Kandau, ambao wanahakikisha kiwango chake kinakua zaidi zaidi siku hadi siku.

# YANGA WEKENI MZIGO MEZANI NIRUDI - MHILU

**Na Adam Fungamwango**

WINGA mshambuliaji wa Kagera Sugar, Yusuph Mhilu, amesema iwapo klabu yake ya zamani Yanga wakifika dau ambalo yeye anahitaji, basi anaweza kurejea kwenye kikosi hicho msimu ujao.

Mhilu ambaye alifunga bao kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake dhidi ya Yanga na wakati zikitoka sare ya mabao 3-3 Jumatano iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, amesema hana matatizo na klabu yake hiyo ya zamani na kama inataka huduma yake, kikubwa tu wamtimizie kile ambacho atahitaji.

"Wakiweka mzigo wa maana ambao mimi nauhitaji narudi, ni makubaliano tu," alisema Mhilu ambaye alifunga bao la tatu kwenye mechi hiyo, lakini pia akiichachafya ngome ya Yanga iliyokuwa ikiongozwa na nahodha Lamine Moro na Bakari Mwamnyeto.

**Mhilu ambaye ni winga, amekuwa mara kwa mara akiifunga timu yake ya zamani ya Yanga na kila anapoifunga huwa hashangilii bao lake.**

"Mimi Yanga ndiyo wamenilea na nakumbuka sana msaada wao kwangu. Ndiyo maana hata nikifunga siwezi kushangilia kwa kuonyesha heshima kwao, ila kufunga ni lazima niwafunge ili kuonyesha kuwa mtoto wao waliyemlea niko kazini kwenye timu nyingine na naendelea kufanya vizuri," alisema Mhilu.

Mchezaji huyo alianzia kikosi cha Yanga B kilichokuwa kikifundishwa na aliyekuwa beki wa zamani wa timu hiyo, Shadrack Nsajigwa, na alipandishwa rasmi mwaka 2016 kikosi cha kwanza hadi mwaka 2018, alipopelekwa Ndanda kwa mkopo wa miezi sita na mkataba wake wa mkopo ulipomalizika, alijiunga na Kagera Sugar ambako amekuwa na kiwango cha hali ya juu kwa sasa.

**WANGU HUU...**




Kipa wa Kagera Sugar, Saidi Kipawa, akijiandaa kudaka mpira huku akizongwa na mshambuliaji wa KMC FC, Charles Ilamfya, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana na KMC kuibuka kwa ushindi wa mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mbeya City malengo pointi za nyumbani*

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Mbeya City, Mathias Lule, amesema mikakati yao kwa sasa ni kupambana kupata pointi 24 kwa kushinda mechi nane za Ligi Kuu watakazocheza kwenye uwanja wao wa nyumbani.

Mechi hizo ambazo Mbeya City inazipigia hesabu ni dhidi ya Dodoma Jiji FC, Mwadui FC, Kagera Sugar, Ruvu Shooting, Coastal Union, Gwambina FC na Biashara United, zitakazopigwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Lule alisema mechi hizo ni muhimu kwao kushinda, na ana matumaini makubwa na wachezaji wake kupata matokeo chanya kulingana na kiwango walichoonyesha katika michezo iliyopita.

Alisema kuna mabadiliko makubwa aliyoyaona katika mechi zao mbili dhidi ya Yanga kwa kutoka sare ya bao 1-1 na kupoteza 2-1 mbele ya Azam FC, hivyo ana imani ya kupata matokeo mazuri katika mechi nane za nyumbani.

"Tunacheza vizuri sana, nina imani kwa kiwango cha wachezaji kikiendelea hivi, basi tuna uwezo wa kupata matokeo chanya kwenye mechi zetu za nyumbani hilo tunalipambania, kwa sababu Tanzania kupata pointi ugenini ni ngumu sana," alisema Lule.

Alisema wana kila sababu ya kupambana kushinda mechi za uwanja wa nyumbani kwa kutafuta pointi tatu na ugenini kwenda kufatufa sare katika mechi zao zilizobaki.

Lule alisema hawako katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi, lakini pia kwa mipango yake ana imani ya timu hiyo kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Kabla ya matokeo ya mechi za jana Mbeya City ilikuwa nafasi ya pili kutoka mkiani na pointi zake 15 sawa na Mwadui FC inayoburuza mkia ambayo ilikuwa ugenini ikicheza dhidi ya Ihefu FC.

Michezo
Jumapili Februari 21, 2021
Nipashe



Man City sasa yamkana Messi UKURASA 22

MSULI MSULI TU...



Viungo wa Simba, Injinia Taddeo Lwanga (kulia) na Hamisi Ndemla katika harakati za kuwania mpira mazoezini. Kikosi cha Simba kinajiandaa na mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa keshokutwa, Jumanne.
**PICHA: MAKTABA**

## Namungo, Waangola vita kali Chamazi leo

**Na Mwandishi Wetu**

NAMUNGO FC na Clube Desportivo 1º de Agosto ya Angola, leo zitakuwa na kibarua kigumu zitakaposhuka katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam kwenye mechi ya awali ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, ambayo Waangola hao watakuwa wenyeji huku wakigharamia kila kitu.

Waangola hao walitua juzi usiku tayari kwa mchezo huo, ambao Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limetoa uamuzi wa mechi zote mbili kuchezwa hapa nchini kutokana na ule wa awali kushindwa kufanyika nchini Angola kutokana na mamlaka nchini humo kuwa chanzo cha kukwamisha kuchezwa.

Kamati ya Mashindano ya CAF ilitoa uamuzi wa mechi hizo mbili hadi kufikia Februari 26, mwaka huu zote ziwe zimechezwa, ambapo kwa mujibu wa ratiba timu hizo leo zitacheza mchezo wa kwanza huku De Agosto wakiwa wageni kabla ya kurudiana Alhamisi ijayo uwanjani hapo Namungo FC ikiwa mwenyeji.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alisema timu yao ipo tayari kwa mechi hiyo na watapambana kuhakikisha wanashinda michezo yote miwili wakianza na wa leo.

"Kwa bahati nzuri tunacheza katika ardhi ya nyumbani mechi zote mbili, hivyo tutatumia faida hiyo kupata matokeo chanya, kwa kubeba pointi zote sita," alisema Zidadu.

# Kocha Al Ahly atabiri vs Simba

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Rekodi yao ushindi na kupoteza ugenini ngoma sare, apata kigugumizi, Gomes naye asema...

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly ya Misri, wakitua nchini juzi usiku tayari kwa mechi yao ya hatua ya makundi ya michuano hiyo dhidi ya Simba, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Pitso Mosimane, ametabiri mchezo mgumu watakapomenyana keshokutwa, Jumanne katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Timu hizo mbili ambazo zipo Kundi A, kila moja imeanza kwa ushindi mechi zao za kwanza, Simba ikiwa ugenini ikiichapa Klabu ya AS Vita ya DR Congo bao 1-0 wakati Al Ahly wakiwa nyumbani waliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan.**

Kuelekea mchezo huo wa Jumanne, baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Mosimane alisema utakuwa mchezo mgumu na wamejiandaa vizuri kuivaa timu hiyo ambayo iliwafunga mara ya mwisho walipokutana Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Tumejiandaa vizuri kuivaa Simba, utakuwa mchezo mgumu, Simba ilitufunga mara ya mwisho tulipokutana hapa, hivyo labda itakuwa wakati wetu wa kusahihisha hilo," Mosimane alimwambia mwandishi.

Alipotakiwa kuzungumzia zaidi nini anachokitarajia kutoka kwa Simba, Mosimane alisema: "Tuwenye furaha kuwapo hapa, tutazungumza zaidi wakati wa mkutano na waandishi wa habari Jumatatu, asante."

Februari 12, mwaka juzi, kwenye mechi ya marudiano ya hatua hiyo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba iliichapa Al Ahly bao 1-0 likifungwa na Meddie Kagere ikiwa ni baada ya mchezo wa awali jijini Cairo, Misri, 'Wekundu wa Msimbazi' hao kukubali kichapo cha mabao 5-0.

Kikosi hicho cha Mosimane, kimewasili nchini bila wachezaji wake watano- Ali Maaloul, Taher Mohamed Taher, Walid Soliman na Salah Mohsen, ambaye ameachwa kutokana na kuwa majeruhi, wakati Hussein El-Shahat akitumikia adhabu.

Hata hivyo, Al Ahly ambao ni mabingwa namba tatu wa Kombe la Klabu Bingwa Dunia, rekodi yao ya kushinda ugenini katika mechi zake 11 za mwisho ilizocheza inalingana ya kupoteza huku kati ya hizo ikitoka sare tatu. Ikiwa ugenini Al Ahly imeshinda mechi nne, kupoteza nne katika michezo 11 za hivi karibuni.

Mechi zake 11 za ugenini ni dhidi ya Simba ya Tanzania 1-0 Al Ahly, AS Vita (DR Congo) 1-0 Al Ahly, Mamelodi Sundowns (Sauzi) 5-0 Al Ahly, Atlabara (Sudan Kusini) 0-4 Al Ahly, Cano (Guinea) 0-2 Al Ahly, Etoile du Sahel (Tunisia) 1-0 Al Ahly, FC Platinum (Zimbabwe) 1-1 Al Ahly, Al Hilal 1-1 Al Ahly, Mamelodi Sundowns (Sauzi) 1-1 Al Ahly, Wydad Casablanca (Morocco) 0-2 Al Ahly, AS SONIDEP (Nigeria) 0-1 Al Ahly.

Akizungumzia mchezo huo, Kocha wa Simba, Mfaransa Didier Gomes Da Rosa, amekiri hautakuwa rahisi lakini akiahidi kupambana ili kupata matokeo nyumbani.

"Kila timu inahitaji kushinda, hivyo hauwezi kuwa mchezo rahisi, lakini malengo yetu ni kupata ushindi kuongezea kile tulichokipata Congo," alisema kocha huyo huku akiongeza kuwa morali ya wachezaji wake iko juu na kila mmoja ana kiu ya kuona wakiibuka na ushindi.

Baada ya mchezo huo, Simba itasafiri hadi Sudan kuifuata Al Merrikh huku Al Ahly ikielekea DR Congo kuwafuata AS Vita, katika mechi ambazo zitapigwa kati ya Machi 5-6, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >